



This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in African Languages*, Volume 2, Issue 1, 2021

Article Information



Submitted: 15th Jan 2021
Accepted: 30th Mar 2021
Published: 4th April 2021

Additional information is available at the end of the article

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

To read the paper online, please scan this QR code



Analysis of face threatening acts on the faces of widows and widowers in funeral context

Judy Nyaboke Nyabuto¹, Francis Kariithi² & Eucabeth Mongare³

Department of Languages, Linguistics & Literature, Kisii University, Kenya

Email: judyNyaboke402@yahoo.com

Abstract

This study intended to identify the acts of speakers that threaten the faces of widows and widowers in funeral condolences. The study was guided by Penelope Brown and Levinson Stephen's Politeness Theory and Ervin Goffman's views on politeness which deals with face issues, face threatening actions and how to save the face from such actions. Population of the study was the speakers who gave condolences to widows and widowers in selected funerals. Descriptive research design guided this study. Purposive sampling was used to identify funerals and speakers. The study employed participant observation as a method of data collection. The study revealed that; despite the fact that speakers tried as much as possible not to threaten the faces of the widows and widowers, sometimes they used words that threatened them especially when they gave complaints, advice, orders and requests to them. The study concluded that if polite language when expressing condolences in a funeral context will be embraced, it will play a big role in respecting the other's privacy and make mourning comfortable among the AbaGusii.

Keywords: condolences, face, face threatening act, politenesses, widows and widowers

How to Cite:

Nyabuto, J. N., Kariithi, F., & Mongare, E. (2021). Analysis of face threatening acts on the faces of widows and widowers in funeral context. *Research Journal in African Languages*, 2(1). Retrieved from <https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/582>

Public Interest Statement

Conversations in the context of funeral is one of the most important aspects in human life, as people in all cultures have an awareness of self-image or "face". This article demonstrates that as much as speakers will try to avoid face threatening acts when expressing their condolences to the widows and widowers, at times they use words that offend and annoy them.



© 2021 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.



This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in Modern Languages and Literatures*, Volume 2, Issue 1, 2021



Article Information

Submitted: 15th Jan 2021
Accepted: 30th Mar 2021
Published: 4th April 2021

Additional information is available at the end of the article

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

To read the paper online, please scan this QR code



Uhakiki wa vitendo vinavyotishia nyuso za wajane katika rambirambi za mazishi

Judy Nyaboke Nyabuto¹, Francis Kariithi² na Eucabeth Mongare³

Idara ya Lugha na Fasihi Chuo Kikuu cha Kisii, Kenya

Email: judynyaboke402@yahoo.com

Ikisiri

Utafiti huu ulinua kuhakiki vitendo vya wahutubu vinavyotishia nyuso za wajane katika rambirambi za mazishi. Utafiti uliongozwa na nadharia ya upole mitazamo ya Penelope Brown, Levinson Stephen na Ervin Goffman inayochunguza masuala ya uso, vitendo vinavyotishia uso na namna ya kuokoa uso kutokana na vitendo hivi. Utafiti ulizingatia muundo fafanuzi. Watafiti walikuwa wahutubu waliopewa nafasi ya kutoa rambirambi zao kwa wajane. Sampuli ya kimakusudi ilitumiwa kuteua mazishi yaliyohudhuriwa na wahutubu. Kati ya wodi (8) katika eneo bunge la Bobasi, 2 (Sameta Mokwerero na Bobasi Boitangare) zilikuwa sampuli ya utafiti. Wodi hizi 2 kila mojawapo ina mitaa 5 jumla ya mitaa 10 ambapo 6 (Etor, Rigo, Kenyerere, Nyamagwa, Igare na Kiongong'i) ilikuwa sampuli ya utafiti ambapo mazishi moja katika kila mtaa yalihadhuriwa jumla ya mazishi 6. Rambirambi zilizosikilizwa na kurekodiwa kama sampuli ya utafiti ni rambirambi za wahutubu 6 katika kila mazishi jumla ya wahutubu 36. Mbinu ya uchunguzi shiriki ilitumika kukusanya data. Matokeo yalidhihirisha kuwa japo wahutubu walijaribu kudumisha nyuso za wajane kwa kuwa makini katika uteuzi wao wa maneno, wakati mwingine walitumia maneno yaliyotishia nyuso za wajane hasa walipowatolea malalamishi, kuwashauri, kuwaamrisha na kuwatolea maombi fulani. Utafiti ulibaini kuwa dhana ya upole ni muhimu wakati wa kuhani na waliofiwa. Utafiti huu ulihitimisha kuwa ikiwa lugha ya upole katika utoaji wa rambirambi itazingatiwa, itachangia pakubwa katika kuheshimu matamania na uhuru wa wengine na kurahisisha maombolezo katika jamii ya AbaGusii.

Maneno muhimu: upole, rambirambi, uso, vitendo vinavyotishia uso, wajane

Utangulizi

1: Usuli wa mada

Sehemu hii imeshughulikia vijisehemu vifuatavyo; dhana ya lugha, rambirambi kwenye sherehe za mazishi, dhana ya upole, jamii ya AbaGusii, utamaduni, vifo na mazishi miongoni mwa AbaGusii na maadili na upole miongoni mwa AbaGusii.

1.2 Rambirambi kwenye sherehe za mazishi

Kwa mujibu wa Kamusi ya *Oxford* (2010), mazishi ni sherehe au ibada inayofanyika kwa muda mfupi baada ya mtu kuaga kukiwamo maziko au kuchomwa kwa mwili wa mfu. Katika muktadha huu, mawasiliano hufanikishwa kutokana na matumizi faafu ya lugha. Halliday (2003) anaeleza kuwa lugha ni mfumo wa maana; yaani mfumo wa ishara. Lugha huwezesha kuwepo kwa maana ambayo huonyesha kuwa mawasiliano yamefanikishwa. Mawasiliano kwa kawaida huwa ni kupashana au kubadilishana mawazo, maoni au habari kwa maneno, maandishi au ishara. Mawasiliano hueleweka vyema wakati mchakato kati ya wahusika wawili una mabadilishano ya fikra, hisia au mawazo ili kufikia lengo au mwelekeo uliokubaliwa.

Mazungumzo kwenye muktadha wa mazishi ni sehemu mojawapo inayochukua nafasi muhimu katika hali zote za maisha ya mwanadamu na hufanikishwa kupitia lugha. Hii ni kwa sababu kifo ni suala zito ambalo husababisha majonzi na kuibua hisia za huzuni zaidi katika maisha ya mwanadamu. Kifo hakiwezi kuepukika na hivyo kinabaki kuwa hali halisi ya maisha ya mwanadamu. Kila wakati watu hufariki na kuwaacha wenzao katika hali ya majonzi, kusunoneka, maombolezo na kukosa tumaini (Bloor na Bloor, 2007).

Sherehe za mazishi hufanywa baada ya mmoja kufariki na hujumlisha shughuli zote za uzikaji (Kamusi Sanifu ya Kiswahili, 2007). Kwa mujibu wa Clark na Labeff (1982), kifo katika jamii hakipangwi na hata mahusiano ya mtagusano wa washiriki katika shughuli za mazishi haidhibitiwi vilivyo. Vifo vimeenea ulimwenguni kote kutokana na majanga mbalimbali kama vile mitetemeko ya ardhi, mafuriko, magonjwa miongoni mwa vianzo vingine vingi. Vifo hivi husababisha sherehe za mazishi kuandaliwa ili kuzika maiti. Waliopatwa na msiba vile vile hushauriwa namna ya kuishi maisha mapya baada ya kufiwa. Shughuli hizi zote za maombolezo na ushauri hutolewa kupitia rambirambi.

Kulingana na Kamusi ya Cambridge (2008), rambirambi ni usemi wa huruma na huzuni unaotolewa kwa familia au marafiki wa karibu wa mtu aliyekufa. Rambirambi huonyesha masikitiko kwa maafa yaliyomfika mtu na mara nyingi huwa ni maneno ya kuwafariji waliokumbwa na msiba. Kupata njia faafu ya kutoa rambirambi wakati wa mazishi huwa ngumu kwa vile msemaji huwa amefungwa na matamano ya kuhifadhi nyuso za waliofiwa (Clark na LaBeff, 1982). Aidha, rambirambi yafaa ziwe za upole ili kupunguza vitisho kwa nyuso za wengine (Mills, 2003). Neimeyer na Gillies (2006) nao wanasema kuwa rambirambi hutolewa kulingana na utamaduni na muktadha wa mwingiliano.

Sherehe za mazishi barani Afrika hufanywa ili kukumbuka maisha ya aliyekufa. Sherehe hizi huleta uhusiano kati ya maisha na kifo huku zikiendeleza kuwepo kwa maisha ya kibinafsi (Capone, 2010 na Nodoushan, 2013). Sherehe hizi zimeenea katika mataifa mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Tanzania na Uganda miongoni mwa mengine.

Nchini Kenya, sherehe za mazishi zimedhihirika katika maeneo mbalimbali kwa mfano Pwani, Nyanza, Bonde la Ufa, Mashariki miongoni mwa maeneo mengine. Jamii kama vile ya Wazaramo, Wakikuyu miongoni mwa zingine hufanya sherehe za mazishi wakati wa kuzika maiti. Jamii ya AbaGusii vile vile ni miongoni mwa zile ambazo hufanya sherehe za mazishi ili kuzika maiti na kuwafariji waliofiwa. Kwa mujibu wa Bloor na Bloor (2007), hali ya huzuni au majonzi wakati wa kifo humkumba aliyefiwa lakini maombolezo huwa ya jumua nzima, hali inayofanya maombolezo kuwa jambo la kiutamaduni. Bloor na Bloor wanaendelea kusema kuwa kama ilivyo mazoea ya kila jamii, maombolezo hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Katika enzi za nyuma, mazishi miongoni mwa AbaGusii yalifanyika nyumbani mwa aliyefariki kwa sababu aliyekufa alikuwa akiishi hapo wakati alikuwa hai (LeVine, 1982) lakini katika kipindi cha sasa mazishi yanaweza kufanyika shuleni, kanisani na katika viwanja vya michezo.

Miongoni mwa AbaGusii mazishi hutazamwa kama sherehe za hadhara ambapo watu hukutana kutoa rambirambi kuhusiana na aliyekufa, kutuliza waliofiwa na kuelezea umuhimu wa maisha kwa ujumla kama ilivyo katika jamii nyingine za Kiafrika (LeVine, 1982). Watu wengi huja pamoja kuonyesha heshima zao kwa aliyekufa kwa njia mbalimbali kama vile kupitia kwa kuimba, kutoa rambirambi, kushiriki katika kazi, kuleta na kupika chakula. Waombolezaji wanapotekeleza shughuli hizi zote hutumia lugha na hivyo husababisha kuwepo kwa jukumu la kuchunguza jamii inavyotumia lugha kutoa rambirambi zao kwa walioathirika na msiba.

Mazishi katika jamii ya AbaGusii husheheni hadhira au waombolezaji wa matabaka tofauti tofauti, jinsia, marika, umri, elimu, hadhi, walio kwenye ndoa na wasio kwenye ndoa. Waombolezaji hawa hutumia lugha kutoa rambirambi zao na hata kuwashauri waliofiwa. Kwa sababu ya tofauti hizi, kuna uwezekano lugha itumike kwa utofauti. Hali hii huleta mtanziko wa kina ambao huenda usiwe bayana namna lugha inatumika na hivyo kuchochea haja ya kuchanganua mikakati ya upole inayotumiwa na wahutubu kudumisha nyuso za wajane wanapotoa rambirambi za mazishi. Aidha, kulikuwa na haja ya kuhakiki vitendo vinavyotishia nyuso za wajane na kuchunguza mikakati inayotumiwa na wahutubu kupunguza vitendo vinavyotishia nyuso za wajane wanapotoa rambirambi zao.

Katika sherehe za mazishi, wahutubu na waombolezaji kwa jumla hutumia lugha kutoa pole zao, rambirambi, kuwafariji na kuwashauri waliofiwa. Wakati mwingi, wahutubu hupata shida wakati wa kutoa rambirambi zao kwa waliofiwa na waombolezaji kwa jumla. Hii ni kwa sababu inakuwa vigumu kuteua mbinu na maneno mwafaka ya kufariji (Clark na LaBeff, 1982). Ili wahutubu waweze kuwasiliana na kushauri, inawalazimu wateue maneno vizuri ili wasije wakawakera waombolezaji na waliofiwa. Lugha ya upole ya kuokoa uso wa msikilizaji ni muhimu katika kufanikisha mawasiliano haya (Brown na Levinson, 1987). Ni kutokana na misingi hii ya kutaka kusetiri uso utafiti huu ulifanywa ili kuhakiki vitendo vilivyotishia nyuso za wajane katika rambirambi za mazishi.

1:3: Dhana ya upole

Kwa mujibu wa Watts (2003), upole ni hulka ya kiasili ya tabia njema. Ni uwezo wa kufurahisha wengine kupitia matendo ya nje ya mtu husika. Anaendelea kueleza kuwa upole ni dhana ya kiakili na kijamii ambayo hukuzwa kupitia mahusiano yetu ya kijamii. Watts hata hivyo

anabainisha kuwa watu hawazaliwi na upole bali wanajifunza kwa kutazama jinsi watu wengine wanatagusana katika jamii yao. Kauli hii inatiwa nguvu na ukweli kuwa dhana ya upole ni tofauti katika jamii na tamaduni. Hii inamaanisha kuwa kinachotambulika na kukubalika kuwa upole katika jamii moja kinaweza kuwa kinyume cha upole katika jamii nyingine.

Upole ni hitaji la kimsingi ulimwenguni kote na utangamano wa watu wote ulimwenguni hudhihirika kupitia matumizi ya lugha (Billow na Krauss, 1988). Billow na Krauss wanaendelea kueleza kuwa ni muhimu kuwa na uelewa wa upole kwa sababu kila wakati wahusika wa mazungumzo wanapotangamana wanajaribu kujielewa kupitia kwa matumizi ya lugha ya upole ili waweze kuhifadhi na kuendeleza mahusiano yao. Kulingana na Billow na Krauss (1988), mawasiliano huvunjika wakati mhusika mmoja katika mawasiliano hutishiwa na aliyemtishia anapokosa kurekebisha au kupunguza vitisho hivyo ili kuzingatia upole.

Upole hudhihirika kutokana na vile watu hujichukulia, namna wanawasiliana na wenzao, jumbe wanazozitumia na matokeo ya jumbe hizo. Wajapani kwa mfano huwa na mawazo maalum kuhusu upole, heshima na aibu. Wao hujaribu wawezavyo ili wasimuudhi mgeni kwa vile jambo hili laweza kuleta aibu kwa mmoja wa wahusika. Utamaduni huu wa upole miongoni mwa Wajapani hudhihirika katika matumizi yao ya lugha kwa sababu wana maneno mengi yanayoonyesha viwango tofauti tofauti vya upole (Troike, 2003). Ni katika kuchanganua lugha inayotumiwa ambapo upole unaweza kudhihirika. Aidha, kuchanganua lugha iliyotumiwa na wahutubu wakati wa kutoa rambirambi ilikuwa njia faafu ya kubainisha vitendo vilivyotishia nyuso za wajane.

Nchini Kenya, upole hudhihirika katika mazungumzo ya aina zote kwa mfano kupitia vipindi vya runinga (Muge, 2018), miktadha ya jandoni (Walubengo, 2010) na katika mawasiliano ya kila siku katika miktadha mbalimbali. Jukumu kubwa la upole nchini Kenya ni kuendeleza utangamano mwema baina ya washiriki katika mazungumzo, kuzingatia hisia za wengine, kujenga uhusiano wa pamoja na kuimarisha mahusiano mema wakati wa mazungumzo.

Miongoni mwa AbaGusii, upole hudhihirishwa kupitia *chinsoni* (sheria za maadili) ambazo huelekeza tabia na utangamano wa watu katika jamii hii (Akama na Maxon, 2006). Sheria hizi huonyesha namna watu wa vizazi na matabaka mbalimbali wanafaa kutangamana katika maisha yao ya kila siku. Kwa mfano, miongoni mwa AbaGusii ilikuwa sheria kuwa wanaume waliooa ndio waliokuwa na msimamo katika familia ambapo waliwatolea wake wao maagizo huku watoto wakichukua nafasi ya chini (LeVine na wenzake, 1994). Hata hivyo, nafasi ya mwanaume katika familia imekumbwa na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya kiuchumi, ukosefu wa ajira na ukosefu wa mwanaume kukidhi mahitaji ya familia yake (Misati, 2015). *Chinsoni* zilipokezwa hasa wakati wa jando na watu wazima walihakikisha kuwa wamewafunza watoto wao kulingana na sheria hizi (Akama na Maxon, 2006). Uzingatiaji wa upole wakati wa mazungumzo ni sheria muhimu sana ili kuendeleza mazungumzo.

1:4 Jamii ya AbaGusii

Levine na Levine (1977), Mayer (1949), Nerlove (1969) na Ochieng (1986) wanabainisha kuwa AbaGusii ni Wabantu wanaoishi katika miteremko ya kusini magharibi mwa milima ya Mau iliyo nyanda za Ziwa Viktoria magharibi mwa Kenya. Wanaeleza kuwa ni jamii inayopakana na Wakipsigis, Waluo na Wamaasai. Wataalamu hawa vile vile wameeleza kuwa AbaGusii walifika eneo hili la kusini magharibi mwa Kenya katikati ya karne ya kumi na nane. Wamefafanua kuwa jamii ya AbaGusii inaishi katika eneo lenye milima na rutuba katika kaunti ya Kisii na Nyamira na wanatumia EkeGusii katika mawasiliano baina yao wanapotekeleza shughuli zao za kila siku.

1:5 Utamaduni

Utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani (Kamusi Sanifu, 2007). Utamaduni hujumuisha tabia zote zinazojidhihirisha na kushirikishwa katika mfumo mzima wa maisha ya wanajamii (Akama na Maxon, 2006). Mathooko (2007) naye anasema kuwa utamaduni ni jumla ya tabia, maadili, maarifa, sanaa, sheria na desturi zinazohitajika na wanajamii wanapoishi na kushirikiana katika jamii. Utamaduni wa jamii ya AbaGusii basi ni uchangamano mzima wa watu wa jamii hii. Utamaduni hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Buliba na wengine, 2006). Utamaduni wa wanajamii fulani huelekeza kwa kiasi kikubwa jinsi lugha inatumiwa na jamii husika. Utamaduni huwezesha kufahamu ni kwa kiasi gani kaida, maadili na kanuni zinavyoelekeza namna lugha inapaswa kutumiwa. Sehemu zifuatazo zinatoa muhtasari wa baadhi ya vipengele vya kitamaduni vya AbaGusii.

1:5:1 Vifo na mazishi miongoni mwa AbaGusii

Kifo huwa ni mojawapo ya sehemu za maisha ambacho hakiepukiki na hivyo kinabaki kuwa uhalisia kwa mwanadamu. Watu hufariki kila wakati na kuwaacha wenzao wakiwa katika hali ya majonzi na maombolezo (Bloor na Bloor, 2007). Katika hali halisi, vifo katika jamii havipangwi ingawa wakati mwingine kuna vile hupangwa hali inayofanya hata mahusiano ya mtagusano wa washiriki katika shughuli za mazishi kutohibitwa vilivyo (Clark na Labeff, 1982). Wakati mgonjwa alipokaribia kufa katika jamii ya AbaGusii, iwapo alikuwa ni mwanamke angewekwa katika *enyomba* (chumba cha ndani) na iwapo alikuwa mwanamume angewekwa *eero* (chumba cha wageni). Baada ya kufariki, sherehe za mazishi ziliandaliwa ili kuzika maiti na kukumbuka maisha ya mwisho ya aliyekufa (LeVine, 1982).

Kifo katika jamii huchukuliwa kama tukio la huzuni na la lazima kwa kila mmoja kwa vile laweza kumkumba yeyote na kwa wakati wowote. Mtu anapokufa, marehemu kwa kawaida anazikwa kulingana na mila na desturi za jamii husika. Shughuli hizi za maziko zinatofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine kukiwemo tofauti za kidini katika utamaduni huo. Aidha, shughuli hizi zinajumuisha imani tofauti tofauti, sala na ibada ambazo zinafanywa kwa heshima ya wafu. Sherehe za mazishi zinaleta uhusiano kati ya maisha na kifo huku zikiendeleza kuwepo kwa maisha ya kibinafsi kwa kutusaidia kupanua uwepo wetu wa kibinafsi. Aidha, sherehe hizi zinaonyesha jinsi ya kuishi maisha mema, kuwa tayari kwa kifo badala ya kukiogopa na zinasaidia kutimisha nia ya pamoja ya kijamii (Capone, 2010 na Nodoushan, 2013 nukuu katika Sahoo, 2014).

Jamii ya Abagusii ni miongoni mwa zile ambazo hufanya sherehe za mazishi ili kuzika aliyekufa na kuwafariji waliofiwa. Bloor na Bloor (2007) wanaeleza kuwa kifo humkumba mtu binafsi lakini maombolezo huwa ya jumuiya yote. Watu wa ukoo wa aliyefiwa (*risaga*) miongoni mwa AbaGusii ndio wangukuja kufanya kazi na walizuiliwa kulima mashamba yao hadi sherehe za mazishi zilipokamilika. Mazishi katika jamii ya AbaGusii yalifanyika nyumbani mwa aliyefariki (LeVine, 1982) lakini katika kipindi cha sasa yanaweza kufanyiwa kanisani, shuleni, sokoni na katika maeneo yaliyotengewa makaburi.

Miongoni mwa AbaGusii, mazishi hutazamwa kama sherehe za kihadhara ambapo watu hukutana kutoa taarifa kuhusiana na aliyekufa na kuelezea umuhimu wa maisha kwa ujumla kama ilivyo katika jamii nyingine za Kiafrika (LeVine, 1982). Katika kuelezea umuhimu wa sherehe za mazishi, Wolfelt (2013) anakubaliana na mawazo ya LeVine (1982) anaposema kuwa sherehe za mazishi ni njia ya jadi na ya kihistoria ambapo jamii huja pamoja kuelezea imani, mawazo na hisia zao juu ya kifo cha mpendwa wao. Wolfelt (2013) anaendelea kusema kuwa miktadha ya mazishi huwapatia waombolezaji ukumbi uliokubalika wa kuelezea hisia zao zenye huzuni na kuwafariji waliofiwa. Kulingana naye, miktadha ya mazishi hualika waombolezaji katika kuzingatia uhusiano wao wa zamani na aliyekufa na kushiriki kumbukumbu hizo na wengine. Aidha, miktadha hii huwapa waombolezaji fursa ya kumkumbuka aliyeaga na kuwasaidia waliofiwa. Katika kuwafariji waliofiwa, waombolezaji wanapaswa kutumia lugha ambayo haibui hisia zozote za huzuni wala kusababisha mkero kwa waliofiwa na hata kwa waombolezaji wengine kwa jumla. Maelezo haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa vile yalisaidia katika uchunguzi wa lugha ya upole iliyotumiwa na wahutubu walipotoa rambirambi za mazishi katika eneo bunge la Bobasi kaunti ya Kisii.

1:5:2 Maadili na upole miongoni mwa AbaGusii

Maadili ni mwenendo mwema au ni onyo au mafundisho yatolewayo kwa nia ya kufundisha (Kamusi Sanifu, 2007). Upole ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mwingine kupitia kutimiza au kuepuka kaida au desturi fulani za mazungumzo (Goffman, 1967). Jamii ya AbaGusii huongozwa na *chinsoni* (sheria za maadili) ambazo huelekeza tabia na utangamano wa watu katika jamii hii (Akama na Maxon, 2006). Akama na Maxon wanaendelea kueleza kuwa *chinsoni* (sheria za maadili) ni mkusanyiko wa sheria ambazo hazijawekwa katika kumbukumbu ambazo huongoza tabia ya AbaGusii. Sheria hizi huonyesha namna watu wa vizazi na matabaka mbalimbali wanavyofaa kutangamana katika maisha yao ya kila siku. *Chinsoni* (sheria za maadili) zilipitishwa kwa vizazi kupitia lugha kwa sababu lugha ni nyenzo muhimu katika uwasilishaji wa utamaduni (Akama na Maxon, 2006).

Uzingatiaji wa madili katika jamii huwawezesha wanajamii kutangamana bila tatizo lolote. Maadili huwafanya wanajamii kutumia lugha isiyokera wala kuudhi wengine. Matumizi ya lugha isiyokera wala kuleta mchafuko wowote wa kihisia kwa wahusika ndio upole (Brown na Levinson, 1987). Upole huundio unaowaongoza washiriki wa mazungumzo kutumia lugha faafu ili kuudhibiti mtagusano baina yao kwa ajili ya kudumisha uhusiano mwema kijamii kama ilivyo katika matumizi ya *chinsoni*. Matumizi ya lugha inayostahili katika mazungumzo huchangia kulinda na kuhifadhi tamaduni za jamii husika.

2: Tatizo la utafiti

Katika utoaji wa rambirambi, upole huhitajika kwa sababu huonyesha heshima za kihisia kwa waliofiwa, huimarisha mahusiano, hujenga heshima na ujasiri na hufanya maombolezo kuendelezwa bila utata wowote. Ili kuzingatia upole na kukuza mlahaka baina ya waliofiwa, wahutubu wanafaa kuteua maneno mwafaka na kwa umakinifu mkubwa kwa kuzingatia mikakati ya upole ili wasije wakawaudhi waliofiwa. Hata hivyo, kuna uwezekano kuwa wahutubu wanapotoa rambirambi za mazishi huenda wakatamia maneno yanayotishia nyuso za waliofiwa. Tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu rambirambi za mazishi zimeegemea uwanja wa Soshiolojia katika mataifa ya kimagharibi kama vile Marekani na Nigeria (Williams, 2006; Ezeifeka na Ogbazi, 2014; Chidimma na Mmadike, 2016). Nchini Kenya, tafiti zilizofanywa kuhusu upole zimejikita katika miktadha ya nyimbo, fasihi andishi, vituo vya redio na runinga (Owino, 2011; Machira, 2015; Hobbs, 2013; Muge, 2018). Kutokana na maandishi yaliyopitiwa, hakuna utafiti uliotalii lugha ya upole katika rambirambi za mazishi kwa wajane katika eneo bunge la Bobasi kaunti ya Kisii. Hili linadhihirisha aidha utafiti kuhusu upole katika rambirambi za mazishi nchini Kenya ulipuuzwa au watafiti hawakuwa na mvuto wa kutafiti katika muktadha huu. Ni kutokana na sababu hizi ambapo utafiti huu ulifanywa ili kuhakiki vitendo vinavyotishia nyuso za wajane katika rambirambi za mazishi.

Lengo la utafiti

Utafiti huu ulilenga kutekeleza lengo lifuatalo;

Kuhakiki vitendo vya wahutubu vinavyotishia nyuso za wajane katika rambirambi za mazishi.

Swali la utafiti

Swali la utafiti lilikuwa;

Je, ni vitendo vipi vya wahutubu vinavyotishia nyuso za wajane katika rambirambi za mazishi?

3: UHAKIKI WA MAANDISHI

Mapitio ya maandishi yaliyofanywa yaliegeme pande mbili ambazo ni tafiti zilizofnywa kuhusu upole na zile zilizofanywa kuhusu rambirambi kwenye mazishi.

3:1: Tafiti Kuhusu Upole

Kuna watafiti wengi ambao wamefanya utafiti kuhusu suala la upole na mikakati yake huku wakitumia nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987). Tafiti zao zilishughulikia matini mbalimbali kama vile nyimbo, sinema, jumbe za simu na kazi bunifu. Tafiti zingine zimejikita katika miktadha maalum kama vile muktadha wa vijana. Muge (2018) alitumia nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) kuchanganua upole katika mazungumzo ya vipindi vya *Sobetab Kapchi* (Maisha ya Jamii) katika idhaa ya KASS FM. Katika utafiti wake, alibainisha kuwa wasemaji wa Kikalenjin ambao walikuwa mashabiki wa kipindi hicho walizingatia upole kama adabu njema na ustaarabu na hivyo kuwapelekea kukumbatia matumizi yake.

Machira (2015) alichambua matumizi ya lugha ya upole kama ilivyotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* ya Walibora (2014). Katika kazi yake,

alichambua jinsi wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* walitumia mikakati ya upole walipotagusana na wahusika wadogo. Alichunguza pia jinsi matumizi ya mikakati ya upole yaliweza kufahamisha sifa za wahusika wakuu na hali zilizoathiri matumizi ya mikakati ya upole miongoni mwa wahusika.

Omosa (2015) alichunguza tasfida kama mkakati wa upole katika Ekegusii na Kiswahili. Anahitimisha kuwa kila lugha asilia ina tasfida zake zisizoweza kutumika au kulazimishwa katika lugha nyingine

Kinyua (2015) alitumia nadharia ya upole kuchanganua ukiukaji wa kanuni za upole katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ya S. A Mohamed. Katika utafiti wake, alitafiti jinsi ukiukaji wa kanuni za upole ulidhihirika katika kauli zilizotolewa na wahusika wakuu, mambo yaliyochochea ukiukaji wa kanuni za upole na namna ukiukaji wa kanuni za upole uliendeleza maudhui katika riwaya hii. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kuwa wahusika wakuu walikiuka kanuni za upole na ukiushi huo ulichochea na muktadha wa mawasiliano, suala lililojadiliwa na hisia za waliozungumza.

Mwari (2014) alishughulikia suala la upole kwa kuchunguza mikakati ya upole katika kipindi cha mawaidha ya Bi. Mswafari katika runinga ya *Citizen* nchini Kenya. Kipindi hiki hupeperushwa na runinga ya *Citizen* kikiwa ni kipindi cha kutoa mawaidha kuhusu ndoa. Mwari alibainisha kuwa suala la upole ni muhimu sana katika mazungumzo kwenye kipindi hiki. Alitambua kuwa vipindi vya runinga hutakiwa kuyajali mahitaji ya nyuso za wahusika katika mazungumzo husika na kukabiliana na vitendo vya kutishia nyuso za wasikilizaji na watazamaji wa vipindi. Aidha, alielezea jinsi mikakati ya upole ilizingatiwa katika kipindi hicho.

Owino (2011) alitumia nadharia ya Brown na Levinson (1987) kuchanganua matini teule za nyimbo za Faustine Munish. Alitumia nadharia hii kutafiti mikakati ya upole namna ilijidhihirisha katika nyimbo mbili za mwimbaji huyu wa nyimbo za kidini. Kutokana na utafiti wake, Owino alitambua kuwa kuna mikakati mbalimbali ya kuokoa uso hasi wa msikilizaji iliyotumika na mwimbaji huyu ili kudhihirisha upole kwa wasikilizaji wa nyimbo zake.

Kariithi (2010) alitumia nadharia ya Brown na Levinson (1987) kuchunguza mikakati ya upole ya lugha ya vijana. Kulingana naye, vijana hutumia lugha inayodhihirisha upole. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kuwa vijana walitumia mseto wa mikakati ya upole katika matumizi yao ya lugha. Aidha, alibaini kuwa mikakati inayotumiwa na vijana hutegemea mhusika, mada na sababu za kuwasiliana.

Habwe (2010) alishughulikia suala la upole katika makala yake *Swahili Forum* 17(2010). Katika kazi hii, alisema kuwa jamii ya Waafrika hupendelea matumizi ya upole wakati wa mawasiliano. Kulingana naye, upole husaidia kudumisha heshima kati ya watu wa vyeo mbalimbali katika jamii. Habwe alisisitiza kwamba lugha inayotumiwa na wakazi wa Nairobi hudumisha upole kinyume na ilivyoaminiwa kuwa mikakati ya upole haizingatiwi na wakazi hao. Anasema kuwa, kwa mujibu wa waasisi wa nadharia ya upole hasa Leech (1983), Brown na Levinson (1987,) upole ni namna ya kuokoa uso wa msikilizaji. Habwe anaendelea kusema kuwa suala la upole ni suala lenye utata kwa sababu linahusu matumizi ya mikakati mbalimbali na wakati mwingine si ya moja kwa moja.

Habwe (2010) alitumia kanuni za Grice (1975) kushughulikia upole katika makala

yake ya *Dialogue drama in Kenyan political speeches and its pragmatic implication* 19(3). Alichunguza jinsi wanasiasa wa Mombasa na Nairobi walitumia mikakati ya upole walipohutubia umati wa watu. Alisema kuwa Kenya ni taifa ambalo limeweka misingi yake kwa vyeo, kabila, dini, utamaduni na rangi hivyo si rahisi kuona mtu aliye na msingi tofauti akipewa kura na watu ambao si wa msingi wake. Kwa sababu ya misingi hiyo, wanasiasa hutumia mikakati mbalimbali ili kuwashawishi wananchi kuwapigia kura.

Hobbs (2003) alitumia nadharia ya Brown na Levinson (1987) kuchanganua lugha ya wanawake na wanaume katika jumbe za simu zilizohifadhiwa katika lugha zungumzwa. Utafiti wake ulibainisha kuwa lugha ya wanawake ilitawaliwa na matumizi ya mkakati chanya wa upole ikilinganishwa na ile ya wanaume. Hobbs alibainisha pia kuwa lugha ya wanawake ilitawaliwa na uombaji wa msamaha na upigaji vijembe walipowasiliana na wenzao wa kiume. Hali hii ilikuwa kinyume cha lugha ya wanaume na hii ni kwa sababu za kijamii kama malezi na utamaduni uliowafanya wanajamii kuwa na majukumu tofauti tofauti kulingana na jinsia.

3:2: Tafiti kuhusu rambirambi kwenye mazishi

Chidimmana Mmadike (2016) walitumia nadharia ya semi tendi ya Searle (1976) kuchanganua semi tendi zilizorudiwarudiwa katika mazungumzo ya mazishi ya Waigbo katika jamii ya Wanaigeria. Katika utafiti huu, waligundua kuwa kauli tendi za ufafanuzi zilitumiwa sana katika sherehe za mazishi. Warambo (2015) alitumia nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi ya Fairclough (1995) na Van Dijk (2005) kuchanganua kwa kina kauli semwa za kisiasa, kijamii na kiuchumi katika rambirambi za mazishi nchini Kenya hasa katika rambirambi zilizotolewa na Junior Odinga wakati wa mazishi ya Fidel Odinga. Katika utafiti wake, Warambo alibaini kuwa katika hafla za mazishi, wahutubu na wanasiasa kwa jumla hudhirisha kauli semwa mbalimbali za kisiasa, kijamii na kiuchumi katika rambirambi zao

Ezeifeke na Ogbazi (2014) walitumia nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi ya Fairclough (1995) na Van Dijk (2005) kuchanganua namna ujane ulijengeka katika jamii ya Waigbo. Katika utafiti wao, walibaini kuwa wajane wa kike hulaumiwa kwa kifo cha waume wao na hili huwafanya kuishi maisha ya kutengwa na familia. Walitafiti katika muktadha wa mazishi sawia na utafiti huu.

Williams (2006) alitumia nadharia ya upole ya Brown na Levinson kuchunguza namna upole ulidhihirika katika utoaji wa rambirambi pale Marekani. Williams alichunguza namna mikakati ya upole ilitumika wakati wa utoaji wa rambirambi na alionyesha namna mahusiano ya kiuwezo yaliathiri uteuzi wa mikakati ya upole iliyotumiwa..

Kutokana na udurusu huu, suala la upole halijatafitiwa katika rambirambi za mazishi kwa wajane katika eneo bunge la Bobasi kaunti ya Kisii nchini Kenya. Utafiti huu ulifanywa ili kuziba Pengo hili katika rambirambi za mazishi kwa wajane ambalo ni ku hakiki vitendo vilivyotishia nyuso za wajane wakati wa kutoa rambirambi.

4: Misingi ya nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya upole hasa mitazamo ya Brown na Levinson (1987) na Goffman (1967) inayochunguza masuala ya uso, vitendo vinavyotishia uso na namna ya

kuokoa uso kutokana na vitendo hivi. Ingawa kuna waasisi wengine waliohakiki nadharia hii kama vile Fraser (1990), Schollon (1995), Spencer (2000) na Watts (2003), mtafiti alichukulia mawazo ya Goffman na Brown na Levinson kuwa toshelevu katika utafiti huu.

Kwa mujibu wa Goffman (1967), upole ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mwingine kwa kutimiza au kuepuka kaida au desturi fulani za mazungumzo na ni mbinu inayotumiwa na wazungumzaji kuheshimiana kimazungumzo ili kudumisha uhusiano wao. Kulingana naye, uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na mtazamo ambao wengine huchukulia kuwa ameegemea katika mtagusano fulani. Goffman anasema kuwa kutunza uso humfanya mtu kuhisi vizuri kwani kunakuwa na uhusiano wa kihisia ambao huhifadhiwa katika hali za kijamii. Kwa madai hayo, watu wanafaa wajaribu kutenda vitendo na kutumia lugha ili kuhifadhi nyuso za wengine kila mara wanapokuwa katika mazungumzo.

Brown na Levinson (1987) wanaangalia upole kama mkakati wa kuokoa uso. Wanaeleza dhana ya uso kama sura ya mtu binafsi ya jamii ambayo mtu huichukulia kuwa yake na kupenda kutambuliwa na yale anayosema. Brown na Levinson walitambua aina mbili za uso wa binadamu ambazo ni uso chanya na uso hasi na kuwa nyuso hizi zinaingiliana. Walieleza nyuso hizi kwa msingi wa mahitaji au matamano ambayo kila binadamu huwa nayo na ambayo huhakikisha kuwa yanathaminiwa. Kulingana nao, wakati tendo la usemi linaenda kinyume na matamano ya uso wa msikilizaji, kunatokea vitendo vinavyotishia nyuso chanya na hasi za washiriki wa mazungumzo. Kulingana nao, uso chanya ni uso ambao unahitaji kupendwa, kukubalika, kuheshimiwa, kuridhiwa na kuhusishwa katika mambo mazuri ya kijamii. Kwa upande mwingine uso hasi ni uso ambao unahitaji kubaki huru. Aidha, waligawa upole katika makundi ya upole hasi na upole chanya na kuweka wazi mipaka ya nyuso hizi mbili kwa kubainisha vitendo vinavyotishia uso chanya na uso hasi wa wahusika katika mazungumzo yoyote. Vitendo hivyo vinaweza kuathiri uso wa msemaji au msikilizaji kwa njia chanya au hasi.

Kategoria ya kwanza ni vitendo vinavyotishia uso chanya wa msikilizaji. Vitendo hivi huathiri hali chanya ya uso wa msikilizaji na humtia aibu msikilizaji. Vitendo hivi humtia ni kama vile: kumkemea msikilizaji, kumdunisha, kumtusi, kumtishia, kutoa malalamishi kwa msikilizaji, kumpinga msikilizaji au kutokubaliana na msimamo wake, kurejelea jinsia ya msikilizaji kwa njia hasi, kuulizia ufafanuzi kutoka kwa msikilizaji, kutaja mada za kimwiko hasa zisizoruhusiwa na utamaduni wa msikilizaji na kumtathmini msikilizaji.

Kategoria ya pili ni vitendo vinavyotishia uso hasi wa msikilizaji. Vitendo hivi hutokea wakati mzungumzaji anapoingilia uso wa msikilizaji bila kupenda kwake. Matendo haya ni kama vile: kuamrisha na kutoa ombi kwa msikilizaji, kumtolea maagizo, kuonya msikilizaji, kutoa ushauri, kutolea msikilizaji mapendekezo, kumkumbusha msikilizaji kuhusu jambo au hali fulani na kudai deni kutoka kwa msikilizaji.

Kategoria ya tatu ni vitendo vinavyotishia uso hasi wa mzungumzaji. Matendo haya hufanyika bila hiari ya mzungumzaji. Vitendo hivi ni kama vile: kukubali ombi la msikilizaji, kukubali mapendekezo ya msikilizaji, kukubali ushauri wa msikilizaji, kukubali shukrani za msikilizaji, kutoa miadi au ahadi kwa msikilizaji bila hiari yake na kukubali wito wa msikilizaji au kukubali kumsamehe msikilizaji.

Kategoria ya nne ni vitendo vinavyotishia uso chanya wa mzungumzaji ambavyo ni kama vile: kukiri makosa mbele ya msikilizaji, kuomba msamaha kutoka kwa msikilizaji, kuomba kutendewa jambo fulani kutoka kwa msikilizaji, kukubali pongezi kutoka kwa msikilizaji, kuomba nafasi kutoka kwa msikilizaji na kujidunisha mbele ya msikilizaji. Utafiti huu ulijikita katika vitendo vinavyotishia uso chanya na uso hasi wa msikilizaji. Mtafiti alichunguza vitendo vilivyotishia uso hasi na uso chanya wa wajane katika rambirambi za mazishi zilizotolewa na wahutubu katika eneo bunge la Bobasi kaunti ya Kisii nchini Kenya.

Ili kukubaliana na hali zinazotishia uso, Brown na Levinson waliweka mikakati ya upole ili itumike wakati wa mazungumzo ndiposa nyuso za wahusika zihifadhiwe. Mikakati hii ni pamoja na mkakati wa upole chanya, mkakati wa upole hasi, mkakati wa kuwa ndani ya rekodi, mkakati wa kuwa nje ya rekodi na mkakati wa kutosema ujumbe unaotishia uso. Nadharia hii inajaribu kurekebisha machukizo au matendo yasiyo ya heshima ambayo huweza kuathiri uso wa mtu. Hujaribu kuokoa uso kutokana na vitendo vinavyotishia uso ambavyo husababishwa na maingiliano ya kijamii. Ili kuwe na maelewano kati ya watu au makundi yanayowasiliana, lazima maneno ya heshima na upole yatumiwe. Nadharia inasisitiza kuwa mawasiliano yoyote hufanikishwa iwapo washiriki wa mazungumzo wanazingatia kanuni za upole kwa makusudi ya kuokoa nyuso zao na za wenzao. Aidha, kila mshiriki wa mazungumzo anatakiwa kuhisi kukubalika na kupewa uhuru wa kutoingiliwa.

5: Muundo na Mbinu Za Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kistahilifu ambao huhusisha upataji maarifa, ufasiri, utoaji maelezo na uchanganuzi kwa mujibu wa jamii husika na mazingira asilia (Creswell na Clark, 2004). Uchunguzi wa kistahilifu hujaribu kutafuta ukweli wa aina tofauti (Kothari 2004). Ni mbinu isiyo na muundo maalum kama katika mbinu ya kihisabati (Maxwell, 2008) bali huhusisha mpangilio bunifu wa kukusanya na kuchanganua data kulingana na madhumuni (Nyandemo, 2007; Flick, 2009). Muundo uliotumiwa ni muundo wa ufafanuzi au wa kimaelezo. Sampuli ya kimakusudi ilitumiwa katika utafiti huu ili kupata data faafu ya kufaulisha madhumuni ya utafiti. Jamii ya AbaGusii ilitiuliwa kimakusudi kwa sababu mtafiti alitaka kufahamu vitendo vinavyotishia nyuso za wajane katika muktadha wa mazishi. Katika jamii hii, mtafiti aliteua eneo bunge la Bobasi katika kaunti ya Kisii nchini Kenya. . Kati ya wodi 8 katika eneo bunge hili, mtafiti aliteua wodi 2 na mitaa yake kuwa sampuli ya utafiti. Wodi hizi ni Sameta Mokwerero mitaa yake ikiwa Etoro, Rigo na Kenyerere na wodi ya Bobasi Boitangare mitaa yake ikiwa Nyamagwa, Igare na Kiongong'i. Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani ambapo mtafiti alihudhuria mazishi ili kukusanya data. Njia iliyotumiwa ilikuwa uchunguzi shiriki ambayo ni njia inayomwezesha mtafiti kujihusisha na watu katika muktadha halisi wa utafiti (DeWalt na DeWalt, 2002). Mtafiti alihudhuria jumla ya sherehe sita za mazishi katika mitaa midogo ya wodi ya Sameta Mokwerero na Bobasi Boitangare katika eneo bunge la Bobasi. Sherehe tatu zilikuwa za wajane walioachwa wa kiume na zingine tatu za wajane wa kike. Nyanjani, mtafiti alinasa hotuba za rambirambi kwa kutumia kinasa sauti na kunakili daftarini kauli zote zilizotishia nyuso za wajane. Katika kila mazishi, rambirambi zilizosikilizwa na kurekodiwa ni sita ambapo tatu zilikuwa za wahutubu wa kike na zingine tatu za wahutubu wa kiume. Jumla ya rambirambi za wahutubu 36 zilizosikilizwa na

kurekodiwa na kuwa sampuli ya utafiti.

Data iliyopatikana baada ya kunasa na kuandika kauli za rambirambi zilizojitokeza ilichanganuliwa sambamba na maudhui kwa maelekezo ya vipengele vya nadharia ya upole. Kauli zilizokuwa katika Ekegusii zilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili zimwezeshe kuchanganua data. Uchanganuzi wa data hii ulifanywa kwa njia ya kimaelezo na majedwali.

6: UCHANGANUZI WA DATA: UHAKIKI WA VITENDO VYA WAHUTUBU VINAVYOTISHIA NYUSO ZA WAJANE KATIKA RAMBIRAMBI ZA MAZISHI

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), kuna matendo ambayo yanaweza kutishia au kukera nyuso za washiriki wa mazungumzo ambao ni msikilizaji na mzungumzaji. Vitendo hivi hutokea wakati wahusika huingiliana na kukinzana katika matamano ya kila mmoja. Hii inamaanisha kuwa baada ya usemi wowote kutolewa au kusikilizwa, msemaji na msikilizaji wanaweza kuathirika kwa njia hasi au chanya kwa pamoja au mmoja baada ya mwingine. Goffman (1959) naye alitambua kuwa katika maingiliano yetu ya kila siku na wengine, kuna nyakati tunapata ugumu wa kuhifadhi nyuso za wengine hali inayopelekea kutokea kwa vitendo vinavyotishia nyuso. Vitendo vya kutishia uso vinavyorejelewa katika utafiti huu ni lugha au usemi usio na heshima au unaoibua hisia za aibu kwa msikilizaji au hali inayomlazimisha msikilizaji kufanya jambo kinyume na matarajio yake. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane katika muktadha wa mazishi, kulidhihirika vitendo vilivyotishia nyuso chanya na hasi za wajane. Vitendo hivyo vilisababishwa na wahutubu kupitia rambirambi zao. Vitendo hivyo vilikuwa kama vifuatavyo:

6:1 Vitendo vinavyotishia uso chanya wa wajane

Vitendo vinavyotishia ni matumizi ya lugha au kauli zinazoweza kuwatia aibu wajane. Vitendo au kauli hizi hutokea wakati hali chanya ya wajane inaathiriwa au inahasiriwa kutokana na kauli zinazotolewa na wahutubu. Hali chanya hapa inamaanisha tamano la kila msikilizaji kupendwa, kusifiwa au kutobaguliwa (Yule, 1996). Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane, vitendo vilivyotishia nyuso chanya za wajane vilidhihirika kama ifuatavyo:

Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha muhtasari wa vitendo vilivyotishia uso chanya wa wajane wakati wahutubu walikuwa wakitoa rambirambi zao katika muktadha wa mazishi.

Jedwali 6:1(a): Muhtasari wa vitendo vilivyotishia uso chanya wa wajane

- Kumdunisha msikilizaji
- Kumtusi au kumsimanga msikilizaji
- Kutoa malalamishi kwa msikilizaji
- Kuzungumzia mambo kuhusu maisha ya msikilizaji kwa namna isiyokubalika

6:1:1 Kumdunisha msikilizaji

Kitendo cha kumdunisha msikilizaji ni mojawapo ya vitendo vinavyoathiri uso chanya wa msikilizaji (Brown na Levinson, 1987). Kudunisha ni kuteremsha thamani ya msikilizaji au ni hali ya kuumbua au kumbeza msikilizaji (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 2007). Hali hii inapodhihirika, uso chanya wa msikilizaji hutishwa. Mifano ifuatayo ilidhihirisha kitendo hicho katika utoaji wa rambirambi kwa wajane. Katika mazishi ya kwanza wodi ya Bobasi

Boitang'are mtaa wa Kiongongi, **MH4** alitumia usemi uliomdunisha msikilizaji ambaye alikuwa mjane **A**(mwanamume) alipokuwa akitoa rambirambi zake. Kauli hiyo ilidhihirika pale ambapo aliuliza mjane kwa nini hakuwambia kuwa dadake alikuwa mgonjwa ili wamshughulikie. Alisema:

EkG: “*Aye mokoyone nabeire ikogosika amatuko amange, nigo watugete omorwaire otanyagototobia? Barisia tibariki gokora igo.*”

Taf: “*Wewe ni shemeji yangu nimekuwa nikikuheshimu kwa siku nyingi, ulikuwa na mgonjwa na hujawahi kutuambia? Dikoni hawafanyi hivyo.*”

Katika mfano huo, kauli **barisia mbariki gokora igo- dikoni hawafanyi hivyo** ilimdunisha mjane **A** kwa kuwa yeye alikuwa dikoni wa kanisa. Mhutu alikuwa anafahamu kuwa mjane huyo alikuwa kiongozi wa kanisa na hivyo alikuwa anajua namna mambo yalifaa kufanywa hasa kuwajulisha watu wakati mtu ni mgonjwa. Mjane angewafahamisha nduguze kuwa dada yao aliyekuwa mkewe alikuwa mgonjwa ili waweze kushirikiana kumtibu. Kwa upande mwingine, huenda uhusiano kati yao haukuwa mzuri ndiyo maana mjane hakuwapasha hali ya dada yao. Mhutu pia alidhihirisha heshima ambayo alikuwa akimpa mjane huyo kupitia kwa kauli **aye mokoyone nabeire ikogosika amatuko amange- wewe ni shemeji yangu nimekuwa nikikuheshimu kwa siku nyingi**. Thamani hiyo iliteremshwa kupitia kwa kauli **barisia mbariki gokora igo- dikoni hawafanyi hivyo** iliyotolewa na mhutu wakati dadake aliugua kwa muda mrefu na hawakuambiwa. Kauli hizo zilipotumika, mhutu aliingilia uso chanya wa mjane **A** hali iliyomfanya apoteze heshima yake na hivyo uso wake ulihasiriwa kutokana na kitendo hicho.

Katika mazishi ya pili wodi ya Sameta Mokwerero mtaa wa Rigo, **MH9** alitishia uso chanya wa mjane **B**(mwanamume) . Wakati alielezea namna shemeji yake ambaye alikuwa mjane **B** alikuwa akijitenga kwa kutowatembelea, kutoingiliana nao wala kuchukua hatua ya kujuana nao, alitumia kauli iliyomdunisha sana. Kauli hiyo ilisababisha aibu kwa mjane huyo na kumfanya adunishwe. Rambirambi zifuatayo zinadhahirisha kauli hayo:

EkG: “*Ing'a akang'ombe akamo ekeri omonto akure nario bono mokorora buna oboiri bwachakire, yaya tari igo*”

Taf: “*Eti kijigombe kimoja wakati mtu amekufa ndio mnajua kuwa uhusiano umeanza, si hivyo.*”

EkG: “*Akang'ombe kari kwaretete akamo iga, toranywoma. Intagete chiombe nonya isato omanyeye konywoma.*”

Taf: “*Kile kijigombe ulileta kimoja tu, hujaoa. Ninataka angalau ng'ombe ndipo uoe.*”

Katika mfano wa kwanza, kauli **ing'a akang'ombe akamo ekeri omonto akure"- eti kijigombe kimoja wakati mtu amekufa** ilitishia uso chanya wa mjane **B**. Kauli hiyo ilimdunisha mjane **B** na kumletea aibu kwa sababu hakuweza kumlipia mkewe mahari wakati alikuwa hai. Hata wakati aliaga, hakuweza kumlipia mahari ya kiwango kizuri bali alitoa ng'ombe mmoja ambaye hakumfurahisha mhutu kwa udogo wake. Hilo lilidhihirishwa na kauli

akagombe akamo- kijigombe kimoja ambayo ilionyesha kuwa ng'ombe huyo alikuwa amekonda sana. Mhutubu alipomwambia mjane huyo hivyo, aliathiri uso wake chanya kwa sababu alimdunisha kwa kutokuwa na uwezo wa kumlipia mkewe mahari yaliyofaa kwa wakati uliofaa.

Aidha, alimdunisha katika mfano wa pili wakati alisisitiza kuwa mjane alitoa ng'ombe mmoja tu kama mahari kwa dadake. Kwa sababu hiyo alimwambia kuwa hajaoa na hivyo alitaka angalau ng'ombe watatu ndio mjane huyo aoe. Hayo yalidhihirika kupitia kwa kauli **akang'ombe kari kwaretete akamo iga toranywoma**"- kile kijigombe ulitoa kimoja tu hujaoa. Kulingana na usemi huo, mwanaume angeheshimika na kukubalika kuwa ameo wakati alikuwa na uwezo wa kumlipia mkewe mahari ya ng'ombe angalau watatu. Alipokosa kufanya hivyo, alidharauliwa na kudunishwa na hiyo ndiyo iliyokuwa maana ya mhutubu huyo kumwambia mjane kuwa hakuwa ameo. Aidha, alitoa ng'ombe mmoja ambaye hakumfurahisha mhutubu hali iliyodhihirisha kuwa mjane huyo hangeheshimiwa. Kauli hiyo ya udunishaji ilipotumika, ilitishia uso chanya wa mjane huyo kwa kuwa ilimwasilisha kama mtu maskini na asiyejali.

6:1:2 Kumtusi au kumsimanga msikilizaji

Kitendo hiki hutokea wakati mzungumzaji anatumia lugha, usemi au maneno ya kukera au kumtusi msikilizaji kwa kumkumbusha aliyofanya au wema aliomfanyia wakati alikuwa na shida kwa lengo la kumuaibisha (Kamusi Sanifu ya Kiswahili, 2007). Kumtusi au kumsimanga msikiliaji ni njia inayodhihirisha kuingiliwa kwa uso chanya na husababisha kuhasiriwa au kutishiwa kwa uso huo (Brown na Levinson, 1987). Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane, wahutubu wengine walitumia maneno ambayo yalionyesha masimango kwa wajane. Mifano ifuatayo inadhihirisha hayo. **MH9** alipotoa rambirambi kwa mjane **B**(mwanamume), alitishia uso chanya wa mjane huyo kupitia usemi wake. Wakati mhutubu huyo alilalamikia mahari ambayo shemeji yake aliyekuwa mjane **B** alikuwa amewapa, alitumia neno lililodhihirisha matusi. Kwa mfano alisema:

EkG: "Buna akang'ombe akamo ekeru omonto akure! Ekio tari ekemira giato, **igo omanyenye toranywoma.**"

Taf: "Eti kijigombe kimoja tena wakati mtu ameaga! Huo si utamaduni wetu, hivyo ujue hujaoa."

Katika mfano huo, kauli **igo omanyenye toranywoma**-hivyo ujue hujaoa ilidhihirisha matusi au masimango kwa mjane **B**. Kauli hiyo ilipotumiwa na mhutubu haikuwa na heshima yoyote kwa sababu kulingana na mila na desturi za msemaji, mwanaume aliheshimika wakati alimlipia mkewe mahari ya ng'ombe zaidi ya mmoja na kwa wakati uliofaa si kungoja hadi wakati wa kifo. Aidha, huenda ilimaanisha kuwa kulingana na sheria, mila, desturi au taratibu za ndoa za jamii ya msemaji(mhutubu), mume aliheshimika kuwa ameo wakati alikubaliana kuishi na mke na kumlipia mahari punde tu ya makubaliano hayo. Mhutubu alipomwambia mjane **B** kuwa hajaoa kwa sababu alitoa mahari ya ng'ombe mmoja ambaye mhutubu hakumwona kuwa wa thamani, alitishia uso chanya wa mjane huyo. Hii ni kwa sababu hadhi na heshima ya mjane **B** iliingiliwa na mhutubu kwa kutomheshimu wala

kumtambua kuwa yeye alikuwa shemeji yake.

MH12 alitumia kauli ambazo zilidhihirisha matusi au masimango alipotoa rambirambi kwa mjane **B**(mwanamume) ingawa hakuzisema katika hali iliyokuwa wazi. Rambirambi ifuatayo inadhihirisha kauli hizo.

EkG: “Kwaigure amangana amange, kwafundishirwe, **bono obongo bwao bwachakire gokora egasi.**”

Taf: “Umesikia maneno mengi, umefundishwa, *sasa ubongo wako umeanza kufanya kazi.*”

Katika mfano huo, kauli **bono obongo bwao bwachakire gokora egasi- sasa ubongo wako umeanza kufanya kazi** ilidhihirisha matusi ingawa hakuisema kwa uwazi. Kila mwanadamu aliyekuwa uhai na mwenye akili timamu, ubongo wake ungekuwa ukifanya kazi. Mhutu alipotumia kauli hiyo alimaanisha kuwa mjane **B** hakuwa na uwezo wa kuamua wala kufanya mambo ambayo yangemsaidia kwa sababu alikuwa amechanganyikiwa kutokana na ugonjwa wa mkewe. Huenda pia alimaanisha kuwa mjane alikuwa amechanganyikiwa alipopata msiba na wakati huo alikuwa ameanza kutulia. Hakumwambia hilo kwa uwazi bali alimwambia mjane kuwa *sasa ubongo wake umeanza kufanya kazi* kudhihirisha kuwa kwa wakati huo mjane aliweza kufanya mambo ambayo yangemwendeleza na angeweza kuwajibika kuwalinda watoto kwa kuwa mkewe alikuwa ameaga. Usemi huo ulipotumiwa uliathiri uso chanya wa mjane huyo hali iliyomfanya kutoheshimika.

6:1:3 Kutoa malalamishi kwa msikilizaji

Brown na Levinson (1987) wanafafanua kuwa ulalamikaji husababisha vitendo vinavyotishia uso wa mhusika katika mazungumzo. Kulalamika ni hali ya kutoridhika na jambo fulani au ni kunung'unika kwa kutoridhika na yaliyofanywa (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 2007). Msemaji au msikilizaji anaweza kunung'unika iwapo yale yanayotendwa au kusemwa hayamfurahishi. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane katika muktadha wa mazishi, wahutubu walilalamika kwa sababu hawakuridhika na yale wajane walifanya. Haya yanabainika katika mifano ifuatayo. Katika mazishi ya kwanza, rambirambi za **MH4** alipotoa rambirambi kwa mjane **A**(mwanamume) zilidhihirisha vitendo vya kutishia uso. Mhutu huyo alitishia uso chanya wa mjane **B** ambaye alikuwa shemeji yake alipomlaumu kuwa hakuwaambia kuwa dadake alikuwa mgonjwa hata baada ya kuugua kwa muda mrefu. Mhutu alilalamika pia kuwa mjane hakumpeleka mgonjwa hospitalini na hata wakati mhutu alishirikiana na ndugu zake wengine kumpeleka hospitalini, mjane huyo alienda pale alipopeleka mgonjwa, akamtoa na kumpeleka hospitali nyingine ambapo mgonjwa hakupata matibabu. Mhutu alimnung'unikia mjane **A** kuwa hakumlinda dadake wala kuwajibika kwa vyovyote ingawa mgonjwa alikuwa ni mkewe. Malalamishi hayo yaliathiri uso chanya wa mhusika huyo kwa kuwa yalimwasilishwa kama mhusika asiyekuwa na utu. Mfano ufuatao unadhihirisha hayo.

EkG: “Bwone nigo ere insaiga lakini timanyeti buna omwana ominto narwarete. **Ekeronaigwete ng'a narwarete, tokamoira togakora ukarabati akarwarigwa**

lakini Monday akairwa 'General Parking'.

Taf: “Kwangu ni hapa karibu lakini sijawahi kuambiwa kuwa dadangu ni mgonjwa. Wakati nilifahamu kuwa ni mgonjwa tulimpeleka hospitali tukafanya juhudi akatibiwa lakini Jumatatu akapelekwa hospitali ya umma ambapo hakutibiwa.”

Mfano huo unadhihirisha kutoridhika kwa mhotubu kutokana na yale yaliyofanywa na mjane **A** kwa dadake. Mhotubu alilalamika kwa sababu walijitolea kumshughulikia dadake ambaye alikuwa mke wa mjane **A** lakini akamficha na kumpeleka hospitali ambayo hakupata matibabu kama ilivyorejelewa na mhotubu kama “*General Parking*” kumaanisha hospitali ya umma. Huenda malalamishi hayo yalimkera mjane huyo kwa vile aliambiwa kile alichokifanya ambacho labda hangetaka watu wajue. Usemi huo ulipotumiwa basi ulitishia uso chanya wa mjane huo kwa kumfanya akereke. **MH11** naye alisababisha vitisho vilivyosababisha kudhuriwa kwa uso chanya wa mjane **B**(mwanamume). Katika rambirambi zake, alimnung'unikia mjane **B** kuwa hakuwahi kuambiwa kuwa dadake alikuwa mgonjwa ingawa alikuwa akiugua kwa muda mrefu takriban miaka kumi. Mhotubu huyo hakuridhika na namna shemeji yake (mjane **B**) alifanya kwa kutowashirikisha katika kumshughulikia mgonjwa. Mhotubu alilalamika kuwa mjane **B** angewafahamisha mapema hata kupitia kwa simu badala ya kungoja hadi wakati dadake alikuwa amekaribia kufa ndipo awaarifu. Malalamishi hayo yalimfanya mjane akereke kwa kuwa yalimletea aibu mbele ya waombolezaji wote. Rambirambi ifuatayo inadhihirisha hayo:

Kisw: “Nilisika uchungu sana kuwa mbona dadangu anakuwa mgonjwa na hatuambiwi, tuko nchi moja hatukuwa Amerika. Ungetafuta nambari yetu utupigie simu, sasa dadangu amekufa kama hana watu wa kwao.”

Katika mfano huo, mhotubu alikereka na kitendo cha kutoambiwa kuwa dadake alikuwa mgonjwa. Hilo lilimfanya anung'unike na kulalamika hadharani kuwa shemeji yake (mjane **B**) hakufanya vizuri. Malalamishi hayo yaliathiri uso chanya wa mjane huyo kwa sababu yamkini yalimfanya audhike na kumsababishia aibu hadharani. Aidha, huenda mjane alikerwa kwa kuwa watu walikuwa wamefahamu kuwa hakuwapasha shemejiye habari za ugonjwa wa mkeo; hali ambayo ingezua maswali mengi kwa watu kuwa kwa nini alifanya hivyo na wangemlaumu kwa kifo hicho.

6:1:4 Kuzungumzia mambo kuhusu maisha ya msikilizaji kwa namna isiyokubalika

Msemaji anapozungumzia mambo yanayohusu maisha ya msikilizaji hadharani bila idhini yake na kwa njia isiyokubalika, huwa anasababisha vitendo vya kutishia kwa uso chanya wa msikilizaji huyo kwa kuwa kutoheshimika au aibu yaweza kutokea. Msemaji anaweza kuingilia uso chanya wa msikilizaji wakati atazungumzia maisha ya msikilizaji hadharani kwa njia hasa kuingilia maisha yake, watoto wake, tajriba yake, kazi yake na hata hali yake ya kiuwezo. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane katika muktadha wa mazishi, wahutubu walizungumzia maisha ya wajane kwa njia isiyokubalika; hali iliyosababisha vitendo vya kutishia kwa nyuso chanya za wajane hao. Rambirambi zifuatayo zinadhihirisha

hayo:

MH8 alitishia uso chanya wa mjane **B**(mwanamume) alipokuwa akitoa rambirambi zake. Alifanya hivyo wakati alizungumzia maisha ya mjane huyo kwa njia isiyokubalika. Mhutubu alielezea namna mjane **B** aliishi maisha ya umaskini hadi kutoweza kukimu mahitaji ya familia yake. Aliendelea kuelezea pia mkewe mjane **B** alivyokuwa akilia wakati wote alipoenda shuleni kumwona mtoto wake aliyekuwa akisomeshwa na mhutubu huyo. Alieleza kuwa mama huyo (mkewe mjane **B**) alilia kwa sababu alikuwa mgonjwa na mumewe (mjane **B**) hakuwa amejitokeza wala kujulikana alipokuwa hadi pale mhutubu alipochukua hatua kumpasha chifu wakashirikiana kumtafuta. Kwa kawaida watu hawataki maisha yao kuingiliwa kwa sababu yanapoingiliwa hali yao inadunishwa na inawaletea aibu. Mhutubu alieleza alivyomsaidia mtoto wa mjane huyo kwa kumpeleka shuleni na kumtafutia mjane **B** kazi ili aweze kuwakimu watoto wengine na mkewe aliyekuwa mgonjwa. Wakati maisha ya mjane huyo yalisemwa hadharani, mjane aliaibika kwa kutokuwa na uwezo wa kukimu familia yake kwa kuwa hakuwa na kazi na hivyo uso wake chanya ulitishiwa. Mfano ufuatao unadhihirisha hayo:

Kisw: “ Nilikaa na mtoto huyu kwa miaka miwili bila wewe kuja shuleni isipokuwa mama ambaye amelala ndiye alikuwa anakuja analia. Nilichukua hatua nikamtafuta chifu akanisaidia kukupata. Nilipokupata ukanielezea shida tutakubaliana nikamchukua mtoto na baada ya wiki mbili nikakutafutia kazi.”

Katika mfano huo, mhutubu alielezea maisha ya mjane huyo hadharani na waombolezaji wote walisikiliza namna mjane aliishi maisha ya kutojiweza na ya kusumbuka kwingi kwa kuwa alikuwa na mgonjwa pia. Mjane huyo labda hangetaka maisha yake yajulikane kwa watu wengi. Hivyo wakati mhutubu aliyaeleza hayo hadharani, huenda mjane alikerwa kwa sababu uso wake chanya uliingiliwa.

Rambirambi za **MH10** kwa mjane **B**(mwanamume) zilidhihirisha vitendo vya kutishia uso chanya wa mjane huyo alipozungumzia maisha ya mjane kwa njia isiyofaa. Mhutubu alielezea namna mjane huyo alisumbuka akiwa hospitalini na hata nyumbani. Alielezea namna watoto wa mjane huyo walikosa chakula hadi ikambidi mjane kwenda vibarua vya pesa kidogo kidogo ili aweze kukimu mahitaji ya familia yake. Mhutubu alipoyaweka maisha ya mjane huyo hadharani, jambo hilo lilimfanya mjane akerwe kwa sababu huenda hakutaka watu wajue alivyokaa. Hilo liliathiri na kuingilia uso chanya wa mjane huyo. Katika rambirambi zake alisema:

EkG: “Rora buna omomura oyo achangegete nonya lunch eborete abana bakori. Omomura oyo arenge koimoka oghenda onyora mia moja iga ogorera abana omogati naende ochiera nyagitari. Rora buna achangegete momororere amabera.”

Taf: “Ona vile huyu kijana alivyosumbuka hata watoto hawapati chakula cha mchana. Kijana huyu alikuwa anafanya vibarua anapata shilingi mia moja

tu anawanunulia watoto mkate na anatomia kwenda hospitalini. Ona vile alisumbuka, mmwonee huruma.”

Katika mfano huo, mhutubu alielezea namna mjane alivyoishi maisha ya usumbufu na ya umaskini. Hakuwa na uwezo wa kuyakimu mahitaji yote ya watoto wake na hata ya mkewe aliyekuwa hospitalini. Mjane huyo alisawiriwa kuwa katika hali ya kusononeka na mwenye mahitaji mengi hadi mhutubu akawaomba waombolezaji wamwonee huruma. Kwa upande mwingine, huenda mjane angeaibika kupokea msaada ambao ungetolewa na waombolezaji kwa sababu hali yake ya umaskini ilikuwa imeanikwa hadharani. Hali hiyo ya kuzungumzia maisha ya mjane hadharani ilileta aibu kwa mjane na hivyo uso wake chanya uliingiliwa.

MH12 alizungumzia maisha ya mjane **B**(mwanamume) kwa namna hasi ambayo ilisababisha vitendo vya kutishia uso chanya wa mjane huyo. Katika rambirambi zake, mhutubu alielezea namna alimsaidia mjane na familia yake kwa kuwapa kazi na mahali pa kuishi. Aidha, alieleza namna mke wa mjane huyo alikuwa amekonda akiwa na tumbo kubwa hali iliyomfanya afikiri kuwa alikuwa mjamzito lakini ilikuwa ni kwa sababu ya ugonjwa. Rambirambi ifuatayo inabainisha hayo:

EkG: “*Nao amenyete bwone ase engecho ye egasi. Nigo achete inkamoa ase akobera amo na abana ... ekeru nachete kobakwania inkanyora **omorugi oye arenge omoreu sana** mbaka inkaeboria omosubati oyo takareeti... nabwate **enda enene ingateba kero kende nigo arosire**”*

Taf: “*Alikuwa akiishi kwangu kwa sababu ya kazi. Alikuwa nikampa pa kuishi na watoto ... wakati nilikuja kuwasalimia nikampata mkewe alikuwa amekonda sana nikajiuliza huyu mwanamke si amekonda sana ... alikuwa na tumbo kubwa nikasema huenda ni mjamzito.”*

Katika mfano huo, mhutubu alimsawiri mjane kuwa alikuwa katika hali ya uhitaji ndio maana alimpa kazi na mahali pa kuishi. Aidha, alizungumzia hali ya mke wa mjane huyo kwa njia isiyofaa kuwa **arenge omoreu sana**- alikuwa amekonda sana na **abwate enda enene**- alikuwa na tumbo kubwa. Kulingana na kauli hiyo, huenda mhutubu alimwona mke wa mjane huyo akiwa katika hali ya kudhoofika kutokana na maradhi, shida au njaa. Huenda pia alimwona kuwa hangemsaidia mjane kutafuta riziki ya kuikimu familia. Mjane alikuwa amepitia hali ngumu kutokana na mkewe kuugua kwa muda mrefu na kukosa kuyakimu mahitaji ya watoto. Huenda mjane hakutaka hali hii izungumziwe kwa vyovyote. Hivyo mhutubu alipoelezea hali hiyo, alisababisha vitendo vya kutishia uso chanya wa mjane huyo kwa sababu kauli alizozitumia zilisababisha aibu na hazikuleta heshima kwa mjane.

MH22 alizungumzia maisha ya mjane **D**(mwanamume) kwa njia isiyokubalika alipokuwa akitoa rambirambi zake. Mhutubu alielezea namna alimsaidia mjane kuoa wakati walikuwa vijana kwa sababu walikuwa marafiki wa karibu sana. Hayo yaliathiri uso chanya wa msikilizaji ambaye alikuwa mjane **D** kwa kuwa huenda hakutaka waombolezaji wajue alivyoa. Katika rambirambi zake alisema:

EkG: “... ase engecho twanchaine korwa tore abana, *ikarora ng’a mbuya inkamotebia nere mbuya amoire nyagosira abe omorugi oye.*”

Taf: “... kwa sababu tulipendana kutoka utotoni, *nikaona ni vyema na nikamwambia ni vizuri amuo marehemu awe mke wake.*”

Katika mfano huo, mhutubu alimsaidia mjane kuoa wakati alikuwa kijana na hilo lilidhihirika kupitia kwa kauli *ikarora nga mbuya ikamotebia nere mbuya amoire nyagosira abe omorugi oye- nikaona ni vyema na nikamwambia ni vizuri amuo marehemu awe mke wake.* Wakati mjane aliambiwa hivyo alikubali na akamuo marehemu kuwa mkewe. Hilo liliashiria kuwa mjane hakuwa na uwezo wa kutafuta mke pekee au hakuweza kukataa. Mara nyingi watu wengi hawataki maisha yao ya ndoa kuingiliwa kwa sababu ndoa ni taasisi inayohitaji kuheshimiwa na kutunzwa. Huenda mjane hakutaka maisha yake ya ndoa yasemwe hadharani na wakati mhutubu aliyasema hadharani, alitishia uso chanya wa mjane huyo kwa sababu mjane huenda angefikiria kuwa kauli ilimsawiri kama mtu mwoga asiyeweza kujitafutia mke. Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha vitendo vilivyotishia uso chanya wa wajane wakati wahutubu walikuwa wakitoa rambirambi zao katika muktadha wa mazishi. Aidha, jedwali linaonyesha idadi ya wahutubu waliotumia vitendo hivyo.

Jedwali 6:1(b): Muhtasari wa vitendo vilivyotishia uso chanya wa wajane na idadi ya watumizi.

Uso chanya	Vitendo vilivyotishia uso chanya	Idadi ya watumizi
	<ul style="list-style-type: none">• Kumdunisha msikilizaji• Kumtusi au kumsimanga msikilizaji• Kutoa malalamishi kwa msikilizaji• Kuzungumzia mambo kuhusu maisha ya msikilizaji kwa namna isiyokubalika	2 2 2 4
	Jumla	10
	Sampuli	36
	Asilimia	27.78

6:2 Vitendo vinavyotishia nyuso hasi za wajane

Vitendo vinavyotishia nyuso hasi ni matumizi ya lugha au kauli zinazosemwa na wahutubu na huwa zinaathiri nyuso hasi za wajane. Vitendo hivi hutokea wakati wahutubu wanaingilia uso hasi wa wajane bila hiari yao. Uso hasi hapa humaanisha hali ya wajane kutaka kubaki huru na kuwa na haki ya kutoingiliwa. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), uso hasi haupendi kuingiliwa kwa vyovyote bila hiari yake. Naye Yule (1996) anadai kuwa uso hasi huhusisha matamano ya mtu kuwa huru, kuwa na uhuru wa kutenda na kuwa na uhuru wa kutolazimizwa na wengine. Wahutubu wanapoingilia uhuru wa wajane wakati wanatoa

rambirambi, huwa wanatishia uso hasi wa wajane hao. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane katika eneo bunge la Bobasi, wahutubu walidhihirisha vitendo vilivyotishia uso hasi wa wajane kwa njia zifuatazo. Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha muhtasari wa vitendo vilivyotishia uso hasi wa wajane wakati wahutubu walikuwa wakitoa rambirambi zao katika muktadha wa mazishi.

Jedwali 6:2(a): Muhtasari wa vitendo vilivyotishia uso hasi wa wajane

- Kuamrisha na kutoa ombi kwa msikilizaji
- Kumtolea msikilizaji maagizo
- Kuonya msikilizaji
- Kumtolea msikilizaji ushauri
- Kumkumbusha msikilizaji kuhusu jambo au hali fulani

6:2:1 Kuamrisha na kutoa ombi kwa msikilizaji

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa mzungumzaji anaweza kuingilia uso hasi wa msikilizaji wakati anaamrisha na kumtolea ombi fulani. Mzungumzaji anapomlazimisha au anapomtaka msikilizaji amtekelezee jambo fulani bila hiari yake, huwa anaingilia uhuru wake na hivyo kuathiri uso hasi wa msikilizaji. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane, wahutubu waliingilia uso hasi wa wajane kwa njia mbalimbali. Mifano ifuatayo inadhihirisha hayo:

MH8 alitishia uso hasi wa mjane **B**(mwanamume) kwa kuingilia uhuru wake. Alitishia uso huo wakati aliamrisha mjane huyo awalinde watoto vizuri na kumwomba aweze kuomba usaidizi wakati wowote angelemewa ili aweze kusaidiwa. Alisema:

EkG: “*Orende abana aba boronge tena ninakusihiki ikiwa umelemewa usiende kando kando au kusema uongo, useme utasaidiwa.*”

Taf: “*Uwalinde watoto hawa inavyostahili tena ninakusihiki ikiwa umelemewa usiende kando kando au kusema uongo, useme utasaidiwa.*”

Katika mfano huo, mhutubu alimuamrisha mjane **B** aweze kuwalinda watoto ilivyostahili na hilo lilidhihirika kupitia kwa kauli “*orende abana aba boronge*”- ulinde watoto hawa inavyostahili. Kupitia kwa kauli hiyo, mhutubu aliingilia uhuru wa mjane **B** kwa sababu mjane alikuwa ndiye baba watoto na alikuwa na haki ya kuwalinda hata asingeambiwa kwa vile lilikuwa jukumu lake. Mhutubu alipomuamrisha awalinde, aliingilia haki yake na aliathiri uso hasi wa mjane huyo. Mhutubu pia alimtolea mjane ombi ambalo alimtaka alitekeleze ambalo lilikuwa kuuliza usaidizi kutoka kwao wakati wowote angepatwa na shida. Huenda mjane hakutaka kuambiwa hivyo wala kutolewa ombi hilo. Inawezekana pia mjane aliwasilishwa kama mtu muongo kutokana na kauli *usiende kando kando au kusema uongo*. Kauli hizo zilipotolewa kwake basi huenda ziliathiri uso wake hasi.

Vitendo vya kutishia uso hasi vilidhihirika katika rambirambi za **MH9** kwa mjane **B**. Alitishia uso hasi wa mjane huyo wakati alimwingilia bila rufusa yake. Mhutubu alipolalamika namna shemeji yake ambaye alikuwa mjane **B** hakuwahi kumpelekea watoto nyumbani kwake ili awajue, alitumia kauli ya kuamrisha ili watoto wapelekwe nyumbani kwake apate kuwajua. Rambirambi ifuatayo inadhihirisha hayo:

EkG: “Bono koru rero iga **intagete ondetere abana aba inka** imbarore erinde imbamanye nonya na amarieta.”

Taf: “Sasa kutoka leo hii, *ninataka uniletee watoto hawa nyumbani* ili niwajue angalau majina.”

Katika mfano huo, mhotubu alimwamrisha mjane ampelekee watoto nyumbani ili awajue. Kauli “**intagete ondetere abana aba inka**”- *ninataka uniletee hawa watoto nyumbani* ilidhihirisha ulazimishwaji ambapo mjane alihitajika afanye alivyoamrisha na mhotubu kwa kuwapeleka watoto nyumbani. Mjane alikuwa na uhuru na haki ya kukaa na watoto wake wasiende popote na huenda hiyo ndiyo iliyokuwa sababu hakuwahi kuwapeleka watoto nyumbani mwa mhotubu. Mhotubu alipomwamrisha mjane awapeleke watoto bila hiari yake, alikuwa ametishia uso hasi wa mjane huyo.

Mfano mwingine ambapo mhotubu huyo aliamrisha mjane **B** ni pale ambapo alimtaka aende kwake ili amfahamu kwa sababu tangu alipomwoa dadake hawakuwahi kujuana naye. Mfano ufuatao unadhahirisha hilo:

EkG: “**Inchwe inka igari inkomanye**”

Taf: “Njoo pale nyumbani nikujue”

Katika mfano huo, “**inchwe inka igari inkomanye**”- *njoo pale nyumbani nikujue* ni kauli amrishi iliyomlazimisha mjane **B** afanye alivyotaka mhotubu. Kwa mujibu wa Yule (1996), matamano na uhuru wa mtu huingiliwa wakati anapolazimishwa na wengine bila hiari yake. Kwa upande mwingine, huenda mjane huyo hakutaka kuamrisha hivyo au aliamrisha bila hiari yake. Hilo lilipofanyika, uhuru wake wa kuamua kama angeenda kwa shemejiye (mhotubu) uliingiliwa na hivyo uso wake hasi ulihasiriwa.

Aidha, mhotubu huyo alipozungumzia kuhusu mahari ambayo shemeji yake (mjane **B**) alikuwa ametoa, alimtolea ombi kwa njia ya kumwamrisha. Alisema:

EkG: “**Intagete chiombe nonya isato** omany konywoma.”

Taf: “*Ninataka angalau ng’ombe watatu ndio uoe.*”

Katika mfano huo, mhotubu hakuridhika na mahari (ng’ombe mmoja) aliyokuwa ametoa shemeji yake (mjane **B**). Kwa sababu hiyo, aliudhika na kumwambia mjane kuwa hajaoa. Ili mjane aweze kuoa, mhotubu alitumia kauli amrishi **intagete-ninataka** ili kumtolea mjane ombi la kumpatia mahari yaliyokubalika na yaliyostahili. Ombi hilo lilidhihirika kupitia kwa kauli **nonya chiombe isato-angalau ng’ombe watatu**. Pengine mjane hakutarajia amri hiyo au ombi hilo kutoka kwa mhotubu. Hivyo mhotubu alipotoa amri hiyo na ombi hilo bila hiari ya mjane, aliuingilia uso hasi wa mjane huyo. Katika rambirambi za **MH10** kwa mjane **B**, kulitokea vitendo vilivyotishia uso hasi wa mjane huyo. Vitendo hivyo vilitokea wakati mhotubu alimwambia mjane awalinde watoto kwanza na ajitolee kanisani ili Mungu amsaidie. Alimwambia hivyo wa kutumia kauli amrishi kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

EkG: “*Korasuki ebiana ebi ... naende ekanisa eria soa ime omogima bi ...*”

Taf: “*Linda vijitoto hivi ... tena ujitolee kabisa kwa kanisa lile ...*”

Katika mfano huo, mhutubu alitumia kauli amrishi **korasuki ebiana ebiga-linda vijitoto hivi na soa ime omogima bi- ujitolee kabisa** kuathiri uso hasi wa mjane huyo. Katika kauli ya kwanza, mhutubu alimtaka mjane awalinde watoto wake kwa sababu walikuwa wachanga na katika kauli ya pili, mhutubu alimtaka mjane ajitolee kanisani kwa kazi ya Mungu ili Mungu amsaidie. Kauli hizo zilimlazimisha mjane kutekeleza yote aliyoambiwa na mjane hali ambayo huenda ilikuwa kinyume na matarajio au matakwa ya mjane. Hivyo kauli hizo ziliingilia uhuru na haki ya mjane kutenda alivyotaka na hivyo ziliathiri uso wake hasi. Aidha, **MH11** alitishia uso hasi wa mjane **B** alipolalamika kuwa shemeji yao (mjane **B**) hakuwaambia kuwa dada yao alikuwa mgonjwa. Katika rambirambi zake, alitumia kauli amrishi kupitisha ujumbe wake kuwa mjane asiutishe uhusiano hata kama dada yake alikuwa ameaga. Rambirambi ifuatayo inaonyesha kauli hiyo:

Kisw: “*Najua dadangu ameaga, kuanzia leo uhusiano usiishe.*”

Katika mfano huo, kauli “**kuanzia leo uhusiano usiishe**” ilimwamrisha mjane asiutishe uhusiano wa kijamaa uliokuwepo kwa sababu ya kifo cha mkewe. Mjane alikuwa na uhuru na haki ya kutenda alivyotaka. Hivyo, uhusiano kati yake na jamaa wa marehemu mkewe ungetegemea maamuzi ambayo angeyafanya. Huenda angeamua kuendeleza uhusiano huo au kuusitisha na hivyo mhutubu alipomwingilia bila kibali chake alitishia uso hasi wa mjane huyo. Vitendo vya kutishia uso hasi vilidhihirika katika rambirambi za **MH26** kwa mjane **E**(mwanamke). Vitendo hivyo vilitokea wakati mhutubu alimwamrisha mjane kuwa asimame imara pamoja na watoto wake kama alivyokuwa mumewe aliyekuwa mwalimu. Mfano ufuatao unadhihirisha hayo:

EkG: “*Omong’ina amo na abana bago stand still buna omwarimu arenge.*”

Taf: “*Mama pamoja na watoto wako msimame imara kama mwalimu.*”

Katika mfano huo, kauli “**stand still**” - *msimame imara* ni amrishi. Kauli hiyo ilimwamuru mjane pamoja na watoto wake waweze kuwa imara alivyokuwa mumewe. Katika rambirambi hiyo pengine mhutubu alimaanisha kuwa mjane na watoto wake wafuate nyayo za mumewe za kuwapenda watu, kushirikiana nao na kusimama katika ukweli wakati wote. Kauli ilimlazimisha kufanya mambo hayo bila hiari kwa sababu alikuwa na uhuru wa kuamua jinsi angeishi na kufanya atakavyo baada ya kifo cha mumewe. Kauli hiyo basi iliathiri uso hasi wa mjane huyo. Katika rambirambi za **MH28** kwa mjane **E**, kulidhihirika vitendo vya kutishia uso hasi wa mjane huyo. Vitendo hivyo vilitokea wakati mhutubu alimwamrisha awe akiwasalimu vile ndugu yake alikuwa akiwasalimu. Alisema:

EkG: “... *otosaguse buna omwarimu arenge gotosagusa.*”

Taf: “... *utusalimu alivyokuwa akitusalimu mwalimu.*”

Katika mfano huo, mhutubu alitumia kauli “**otosaguse buna omwarimu arenge gotosagusa**”- *utusalimu alivyokuwa akitusalimu mwalimu* kumwamrisha mjane kuwa aendelee uhusiano aliokuwa nao mumewe ambaye ni kakake. Kwa upande mwingine, pengine mhutubu alimaanisha kuwa mjane aendelee kuwasaidia alivyokuwa akiwasaidia kakake. Kauli hiyo ilimwingilia mjane kwa kuwa huenda hakutaka kuambiwa hivyo au hakutaka kuendeleza uhusiano huo wala kuwasaidia kwa vile mumewe alikuwa ameaga. Kauli hiyo ilipotumiwa, uso hasi wa mjane huyo ulitishiwa kwa kuwa uhuru wake wa kuamua kile angefanya uliingiliwa. Mhutubu huyu vile vile aliutishia uso hasi wa mjane huyo wakati alimtolea ombi ambalo alilitaka alitekeleze. Alimtolea ombi hilo wakati alimtaka mjane aulize ushauri namna angeishi. Mfano ufuatao unadhihirisha hilo:

EkG: “... *bamura bamino imbaroo, baborie ushauri ...*”

Taf: “... *ndugu zako wako, waulize ushauri ...*”

Katika mfano huo, mhutubu alidhihirisha ombi ambalo alitaka mjane alitekeleze kupitia kwa kauli “**baborie ushauri**”- *waulize ushauri*. Kauli hiyo ilikuwa ya kumwamrisha mjane afanye namna mhutubu alitaka bila hiari yake. Huenda mjane hakutaka ushauri wowote kutoka kwa nduguze hata kama mumewe alikuwa ameaga. Mhutubu alipomtolea ombi hilo bila hiari yake, aliuingilia uhuru wake na hivyo alitishia uso hasi wa mjane huyo. **MH30** naye aliutishia uso hasi wa mjane **E**(mwanamke) wakati alimwambia kuwa arudie maisha aliyokuwa akiishi hapo awali. Alisema:

EkG: “*Nigo ikogosaba oirane ase obogima boria mwamenyete kare amakueri tabaisa kobaturubania, mobwaterane na abana Nyasae abae ebisio.*”

Taf: “*Ninakuomba uyarudie maisha mliyokuwa mkiishi hapo awali, kifo kisiwasambaratishe, mshirikiane na watoto Mungu awabariki.*”

Katika mfano huo, kauli “**oirane ase obogima boria mwamenyete kare**”- *uyarudie maisha mliyokuwa mkiishi hapo awali* inadhihirisha ombi la mhutubu kwa mjane. Kauli nyingine “**mobwaterane na abana**”- *mshirikiane na watoto* ni amrishi. Mhutubu alikuwa anamtaka mjane aendelee kuishi maisha ya ukristo na asijichanganye na maovu ya dunia kama walivyokuwa wakiishi wakati mumewe alikuwa hai. Aidha, alimtaka mjane ashirikiane na apendane na watoto wake ili waweze kufanikiwa na waishi kwa amani. Kauli hizo zilitolewa bila hiari ya mjane kwa sababu mjane alikuwa na uhuru na haki ya kuishi apendavyo bila kuingiliwa. Mhutubu alipouingilia uhuru wa mjane namna hiyo, aliutishia uso wake hasi. Rambirambi za **MH32** kwa mjane **F**(mwanamke) zilidhihirisha vitendo vya kutishia kwa uso hasi wa mjane huyo. Vitendo hivyo vilitokea wakati mhutubu alimwamuru mjane awe na upendo na awatembelee ili ajue mahali walikuwa wakikaa. Alimtolea kauli hiyo ili aweze kuendeleza uhusiano uliokuwepo baina yao na nduguye (mume wa mjane) aliyekuwa

ameaga. Alisema:

EkG: “*Omong’ina gwatigaire enka eye **obe no obwanchani, omany chinka chiato na abana batomanye ase tore imbatweba.***”

Taf: “*Mama ambaye umebaki katika mji huu uwe na upendo, ujue nyumbani mwetu na watoto wajue mahali tunakaa wasitusahau.*”

Katika mfano huo, mhutubu alimwamrisha mjane awe na upendo kama ilivyoidhihirika kupitia kwa kauli “**obe no obwanchani**”- uwe na upendo. Kulingana na kauli hii, huenda mjane pamoja na mhutubu aliyekuwa shemeji yake hawakuwa wanasikizana au kuwa na uhusiano mwema. Aidha, mhutubu alimwamrisha awatembelee kama ilivyobainika kupitia usemi “**omany chinka chiato**”-ujue nyumbani mwetu na awaruhusu watoto wawatembelee nyumbani kwao kama ilivyobainika kupitia kwa kauli “**abana batomanye ase tore**”-watoto wajue mahali tulipo. Pengine ilikuwa ni kutokana na kutokuwepo na uhusiano mwema kati yao ndiyo sababu mjane hakutangamana na mhutubu wala kuwaruhusu watoto wake wawatembelee. Rambirambi hiyo pia ilimaanisha kuwa mjane aendeleze uhusiano wa kifamilia baina yake na dada zake marehemu mumewe. Mhutubu alikuwa na haki ya kuendeleza maisha yake alivyotaka na alikuwa na uwezo wa kutowaruhusu watoto kwenda kuwatembelea shangazi wao (mhutubu na dadake). Mhutubu alipomtolea mjane kauli hizo bila hiari yake, aliathiri uso hasi wa mjane huyo kwa kuingilia uhuru na haki yake.

6:2:2 Kumtolea msikilizaji maagizo

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), utoaji wa maagizo kwa msikilizaji ni kitendo kinachoathiri uso hasi wa msikilizaji. Ili kitendo hiki kibainike, mzungumzaji anatumia maneno agizi yanayomtaka msikilizaji afanye jambo fulani bila hiari yake. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane, wahutubu mbalimbali waliwatolea wajane maagizo bila idhini yao na hivyo kusababisha vitendo vya kutishia uso. Mifano ya rambirambi ifuatayo inadhihirisha vitendo hivyo: Rambirambi za **MH1** kwa mjane **A**(mwanamume) zilidhihirisha vitendo vya kutishia uso hasi wa mjane huyo. Vitendo hivyo vilitokana na maagizo ambayo mhutubu alimtolea mjane huyo kuwa awe mvumilivu katika maisha na amwamini Mungu. Mfano ufuatao unabainisha maagizo hayo:

EkG: “*... beka ogosemeria kwago ase omotongi oito.*”

Taf: “*... weka tumaini lako kwa muumba wetu.*”

Katika mfano huo, mhutubu alimtaka mjane aweke tumaini lake kwa Mungu kwa sababu ndiye angemsaidia. Maagizo hayo yalidhihirika kupitia kwa kauli “**beke ogosemeria kwago ase omotongi oito**”- weka tumaini lako kwa muumba wetu. Maagizo hayo yangeweza kumuudhi mjane iwapo yalitolewa bila idhini yake au iwapo hakuyaafiki. Hivyo mhutubu alipomtolea maagizo hayo kinyume na matarajio yake, aliathiri uso wake hasi. **MH3** alitishia uso hasi wa mjane **A** wakati alimtolea maagizo kuwa awalinde watoto wake vizuri na kuuliza ushauri kutoka kwa ami zake wakati wowote ule angepatwa na shida. Katika rambirambi zake alisema:

EkG: “*Abana gwatigeirwe nabwo okoba ange ... moche amo, abaisomoke imbaroo ekeru kwanyorire obokongu kwababoria nabo bakogokonya.*”

Taf: “*Watoto ulioachiwa uwalinde ... muungane, ushauriane na ami zake wakati umekumbwa na shida watakusaidia.*”

Katika mfano huo, mhutubu alimpa mjane maagizo matatu ambayo alitaka ayatekeleze. Agizo la kwanza lilikuwa kuwalinda watoto kama ilivyodhihirika kupitia kwa kauli “*abana gwatigeirwe nabwo okoba ange*”- watoto ulioachiwa uwalinde. Agizo la pili alimtaka mjane pamoja na watoto wake wapendane, waelewane na waungane kama ilivyodhihirika kupitia kwa kauli “*moche amo*”- muungane. Agizo la tatu lilikuwa mjane atafute ushauri kutoka kwa ami zake wakati wowote angepatwa na shida na hilo ni dhahiri katika kauli “*abaisomoke mbaroo ekeru kwanyorire obokongu kwababori*”- ushauriane na ami zake wakati umekumbwa na shida. Kwa kawaida watu hujaribu kuweka siri mambo ya kifamilia au tabia za watoto wao hasa mienendo mibaya. Kwa sababu hiyo, huwa vigumu kuuliza ushauri kutoka kwa mtu kwa kuopa kuwa huenda siri hizo zikafichuka na kuenea kwa watu wengine. Vile vile huenda mjane angepata ugumu wa kuuliza ushauri kutoka kwa ami zake wakati angepata shida kama hakutaka kufanya hivyo. Mhutu alipomtolea mjane maagizo hayo, aliingilia uso hasi wa mjane huyo kwa sababu huenda mjane hangeafikiana na maagizo hayo au hakuyahitaji.

Rambirambi za **MH10** kwa mjane **B** zilidhihirisha vitendo vilivyotishia uso hasi wa mjane huyo alipomtolea maagizo kuwa awalinde watoto na awakuze wawe na mienendo mizuri kwa sababu ndiyo wangemsaidia. Kutokana na rambirambi hiyo, huenda mjane angefasiri kuwa hakuwalinda watoto hao wakati mkewe alikuwa hai. Aidha, angeweza kuifasiri kuwa watoto wake hawakuwa na hulka njema na hivyo alifaa awakuze vyema kama ilivyodhihirika kupitia kwa kauli *orende abana aba- ulinde hawa watoto na bakine buya- wakue na tabia nzuri*. Iwapo angefasiri rambirambi hiyo kwa njia hasi, bila shaka uso wake hasi ungeathirika. Aidha, maagizo hayo ya kuwakuza watoto pengine yalimkera kama hakuyahitaji au yalitolewa bila hiari yake. Haya ni kwa msingi kuwa alikuwa na uhuru na haki ya kuwalinda watoto wake kwa njia ambayo angeiona kuwa bora hata bila kuambiwa. Rambirambi ifuatayo inadhihirisha hayo.

EkG: “*... orende abana aba Nyasaye agosesenie bakine buya*”

Tafsiri: “*... ulinde hawa watoto Mungu akubariki wakue na tabia nzuri.*”

MH12 alitishia uso hasi wa mjane **B** wakati alimtolea maagizo kuwa afanye kazi kwa sababu alikuwa amefahamishwa kuwa alihitaji kuilinda familia yake kwa njia iliyofaa. Katika rambirambi zake alisema:

EkG: “*... kwabundisirwe bono obongo bwago bwachakire gokora egasi. Bono kora egasi, ekio nakio indagotebie.*”

Taf: “*... umefundishwa, sasa ubongo wako umeanza kufanya kazi. Sasa fanya kazi,*”

hayo ndiyo nitakwambia.”

Katika mfano huo, kauli “**bono kora egasi**”- *sasa fanya kazi* ni kauli agizi iliyodhihirisha kuwa mjane alihitajika afanye kazi au atie bidii sana zaidi ya alivyokuwa akifanya hapo awali wakati mkewe alikuwa hai. Kauli hiyo huenda iliathiri uso hasi wa mjane kwa sababu mjane alikuwa akifanya kazi na akiwa baba watoto, alifahamu kuwa alifaa kufanya kazi ili ayakimu mahitaji ya watoto wake kwa sababu ndiye alikuwa amebaki kama mzazi wa kipekee. Huenda pia hakutaka kuagizwa hivyo kwa kuwa hilo lilikuwa jukumu lake la kawaida. Mhutu alipomtolea mjane maagizo hayo basi huenda aliutishia uso hasi wa mjane huyo kwa kuingilia uhuru wake wa kufanya alivyotaka. Katika mazishi ya nne, rambirambi za **MH20** kwa mjane **D**(mwanamume) zilidhihirisha vitendo vya kutishia uso hasi wa mjane huyo wakati alimwaagiza kuwa avumilie na amtegemee Mungu zaidi kwa sababu watu walikuwa wengi waliokuwa wameachwa wajane kama yeye. Alisema:

EkG: “*Naintwe itwatigetwe ababoraka, bono soa ase ebikoroto ebi obibeke otegerere lakini egento ekenene bwebange gochi ase Nyasae.*”

Taf: “*Nasi tuliachwa wajane, sasa valia viatu hivi utulie lakini jambo la muhimu umwamini Mungu.*”

Katika mfano huo, mhutu alimtolea mjane maagizo mawili aliyotaka ayatekeleze. Agizo la kwanza lilikuwa ayakubali na kuyavumilia maisha ya ujane kama ilivyobainika katika kauli “**bono soa ase ebikoroto ebi obibeke otegerere**”- *sasa valia viatu hivi utulie*. Agizo la pili lilikuwa atengeneze mapito yake yawe sawa kwenda kwa Mungu kwa kumwamini na kumtegemea kama ilivyobainika katika kauli “**bwebange gochi ase Nyasae**”- *umwamini Mungu*. Kauli hizo huenda ziliathiri uso hasi wa mjane huyo iwapo zilitolewa kinyume na matarajio yake au bila hiari yake. Rambirambi za **MH21** kwa mjane **D**(mwanamume) zilidhihirisha vitendo vilivyotishia uso hasi wa mjane huyo. Vitendo hivyo vilitokea wakati mhutu alimtaka mjane huyo awalinde watoto hasa yule aliyekuwa mdogo na aweze kuulinda mji. Katika rambirambi zake alisema:

EkG: “*... oagate nka eye na orende abana aba kobua mono oyo omoke ekiagera abande bakinire.*”

Taf: “*... ukumbatie mji huu na uwalinde watoto hawa hasa huyu mdogo kwa sababu wengine wamekuwa wakubwa.*”

Katika mfano huo, mhutu alimtolea mjane maagizo mawili; agizo la kwanza lilikuwa aulinde mji na la pili awalinde watoto hasa yule aliyekuwa mdogo. Katika mfano huo, maagizo ya mhutu kwa mjane yalikuwa ya kumlazimisha hasa katika agizo la kuwalinda watoto. Alipotumia kauli **kobua mono oyo omoke**- *hasa huyu mdogo*, alisisitiza ujumbe huo na mjane alifaa afanye kulingana na vile alivyoagizwa. Kwa mujibu wa Yule (1996), uso hasi huhusisha matamano ya mtu kuwa huru, kuwa na uhuru wa kutenda na kuwa na uhuru wa kutolazimishwa na wengine. Mhutu alipomtolea mjane maagizo hayo, huenda aliathiri

uso hasi wa mjane huyo kwa sababu mjane alikuwa na haki ya kuishi apendavyo na kuwalea watoto wake kwa njia ambayo angeiona kuwa bora hata bila kuambiwa kwa vile hilo lilikuwa ni jukumu lake. Vitendo vya kutishia uso pia vilibainika katika rambirambi za **MH24** kwa mjane **D**. Vitendo hivyo vilitokea wakati mhutubu alimtolea mjane maagizo kuhusu alivyofaa kushirikiana na watoto wake, kuwalinda na kuwakosoa ili waweze kuendeleza kizazi cha marehemu dadake. Rambirambi ifuatayo ilibainisha hayo:

EkG: “... etimu gwatigeirwe **kora nero esemina**, eyio nero bono **okobwaterera bokong’u ogororokie omochie** ‘omosubati ominto.”

Taf: “... timu uliyoachiwa **fanya nayo semina**, ishikirie kabisa ili uendeleze mji wa dadangu”

Katika mfano huo, mhutubu alimtaka mjane awalee na kuwakuza watoto wake kwa njia nzuri. Mjane alifaa ashirikiane na watoto hao, awape mawaidha ambayo yangewafaa na awarekebishe kwa kuwakosoa kila wakati. Haya yalibainika katika kauli “**kora nero esemina**”- *fanya nayo semina* na ashirikiane nao kama ilivyodhihirika katika kauli “**okobwaterera bokong’u**”- *uishikirie kabisa*. Neno semina hapa lilimaanisha kuwa mjane akae na watoto wake awafundishe kwa kina maadili ambayo yangewawezesha kukabiliana na hali tofauti tofauti za maisha. Maagizo hayo huenda yaliuingilia uhuru na haki ya mjane kwa sababu huenda hayakumpa nafasi ya kufanya alivyotaka na hivyo yalitishia uso wake hasi. Uso hasi wa mjane **E**(mwanamke) ulitishiwa wakati **MH27** alikuwa akitoa rambirambi zake. Mhutubu huyo alifanya hivyo wakati alimwagiza mjane aungane na watoto wake ili maisha yao yaweze kuwa rahisi. Mfano ufuatao ulidhihirisha hayo:

EkG: “Omong’ina **mobe amo na abana moigwane** kende tikeiyo kerasinye.”

Tafs: “Mama muungane na mpendane na watoto, kila jambo litakuwa rahisi.”

Katika mfano huo, mhutubu alitumia kauli agizi “**mobe amo na abana moigwane**”- *muungane na mpendane na watoto* kumwagiza mjane atende alivyomwambia. Huenda mjane hakutaka kuambiwa hivyo kwa sababu alikuwa na uhuru wa kuwalinda na kushirikiana na watoto wake hata bila kuambiwa. Mhutubu alipomwambia hivyo bila kibali chake huenda aliuingilia uso wake hasi na hivyo kuuathiri. Rambirambi za **MH28** kwa mjane **E**(mwanamke) zilidhihirisha vitendo vya kutishia uso hasi wa mjane huyo. Vitendo hivyo vilibainika wakati alimwagiza mjane ashirikiane na wenzake na aendelee kuonyesha uelewano huo kila wakati. Rambirambi ifuatayo inadhihirisha hayo:

EkG: “... **mobwaterane amo na abamino ase kera ringana**. **Moigwane** naende **mogenderere koorokia okoigwana oko**.”

Taf: “... *mshirikiane na wenzako* kwa kila jambo. Muelewane na mwendelee kuonyesha uhusiano huu.”

Katika mfano huo, kauli “**mobwaterane amo na abamino ase kera ringana**”- *mshirikiane na*

wenzako kwa kila jambo, “**moigwane**”- muelewane na “**mogenderere koorokia okoigwana oko**”-mwendelee kuonyesha uhusiano huu ni agizi. Mhutubu alitumia kauli hizo kumwagiza mjane afanye alivyotaka. Kwa upande mwingine, mjane alikuwa na uhuru wa kuamua vile angeishi baada ya mumewe kuaga hata bila kuelekezwa. Huenda pia mjane hakutaka kuambiwa namna hiyo na hivyo mhutubu alipomwambia hivyo, kulikuwa na uwezekano kuwa aliutishia uso wake hasi kwa kuingilia uhuru na haki yake.

6:2:3 Kuonya msikilizaji

Mzungumzaji anaweza kutishia uso hasi wa msikilizaji wakati anamuonya dhidi ya jambo fulani bila idhini yake. Kuonya ni kumwelekeza mtu kupitia maneno au kumkataza mtu kwa kumwonyesha hatari itakayotokea (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 2007). Kawaida, huwa vigumu kwa watu kupokea onyo kwa sababu onyo mara nyingi huhusishwa na matendo hasi (Brown na Levinson, 1987). Mtu huonywa wakati ametenda au amesema kauli hasi au huonywa kabla ya kutenda au kusema kauli hasi ili aache. Kumwonya mtu husababisha aibu na huingilia uhuru na haki ya mtu ya kutaka kufanya atakavyo. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane, wahutubu waliwaonya wajane dhidi ya hali na mambo mbalimbali kama inavyobainika katika mifano ifuatayo. Katika mazishi ya pili wodi ya sameta Mokwerero mtaa wa Rigo, **MH7** na **MH10** walitishia uso hasi wa mjane **B**(mwanamume) walipomwonya dhidi ya kuoia tena. Walimwonya kuwa asiharakishe kuoia tena bali awalinde watoto kwanza kwa sababu walikuwa wachanga. Aidha, walimwonya kuwa hakukuwa na mwanamke ambaye angewalinda watoto hao vyema kama mkewe aliyekuwa ameaga. Walipotoa rambirambi zao walisema:

EkG: “Egento inkogokurera mono **toayerera konywoma, orarenda abana aba.**”

Taf: “Ninakuonya tahadhari sana, *usiharakishe kuoia tena, linda hawa watoto kwanza.*”

EkG: “**Tobaisa kong’aineka ogende ng’a konywoma ore, mokungu onde tari orache arende amwana buna oyo omoke.**”

Taf: “*usije ukadanganyika ukaoia tena, hakuna mwanamke atakuja alinde mtoto kama huyu mchanga.*”

Katika mifano hiyo, wahutubu walimwonya mjane kwa kumtahadharisha kuwa asiharakishe kuoia tena kama ilivyodhihirika katika mfano wa kwanza kupitia kauli “**toayerera konywoma**”- usiharakishe kuoia na **tobaisa kongaineka ogende nga konywoma ore**”- usije ukadanganyika ukaoia tena katika mfano wa pili bali awalinde watoto kwanza na hili lilikuwa dhahiri katika kauli “**orarenda abana aba**”- linda hawa watoto kwanza. Kulingana na rambirambi ya kwanza, mhutubu hakumkataza mjane kuoia tena bali alimkanya kuwa awalinde watoto kwanza ili watakapokuwa wakubwa angeweza kuoia tena. Katika rambirambi ya pili, mhutubu alimtaka mjane ajaribu kuepuka ubaya au hatari ambayo ingetokea iwapo angeoia tena. Ubaya au hatari hiyo labda ingekuwa kuwa mjane huenda angesahau wajibu wake kwa watoto na kuwaacha wasumbuke au mke ambaye angeoia angewatesa. Kauli hizo ziliposemwa kwa mjane, kulikuwa na uwezekano zimkasirishe

kwa sababu huenda hakuwa na nia ya kuoia tena au hakutaka aonywe hadharani hivyo. Kauli hizo basi zilitishia uso hasi wa mjane huyo kwa kumfanya asiwe na uhuru wa kufanya alivyotaka. Kuna uwezekano kuwa **MH11** alipotoa rambirambi kwa mjane **B**, aliutishia uso hasi wa mjane huyo. Alifanya hivyo wakati alimwonya dhidi ya kuoia tena msichana kutoka kwa jamii yao. Alimwonya kwa sababu hakuweza kumlinda marehemu dadake aliyetoka katika jamii hiyo. Alisema:

Kisw: “Ninaomba huyu shemeji yangu, kosa ambalo ulifanya **na siku moja usirudie kupata msichana kutoka huko.**”

Katika mfano huo, mhutubu alitambua kosa alilolifanya mhutubu ambalo lilikuwa kuoia kutoka jamii ya Waluo. Ilikuwa ni kwa sababu hakumlinda msichana (dadake) aliyeoa kutoka jamii hiyo, hivyo alimwonya mjane kuwa mtu ambaye hakuwajibika kumlinda mkewe. Kwa sababu hiyo, alimwonya kupitia kauli **na siku moja usirudie kupata msichana kutoka huko** ili asiweze kurudia kosa alilokuwa amelifanya hapo awali. Kwa upande mwingine, mjane alikuwa na uhuru na haki ya kutenda alivyotaka, hivyo mhutubu alifaa kuheshimu uhuru huo kwa kutomwingilia kwa vyovyote, lakini alipomwingilia kwa kumwonya hadharani, aliutishia uso hasi wa mjane huyo. Rambirambi za **MH35** kwa mjane **F**(mwanamke) zilidhihirisha vitendo vilivyotishia uso hasi wa mjane huyo. Vitendo hivyo vilibainika wakati mhutubu alimwonya kuhusiana na kifo cha mumewe. Mhutubu alimwambia mjane aelewe kuwa kifo cha mumewe kilisababishwa na shetani wala haikuwa mtu yeyote. Mfano ufuatao unabainisha hayo:

EkG: “... *onde takong’aina ng’a eke ikiarengo gose inyarebe omorogete, onye ngwachiete aande konang’a ikwamobwenetie, manya ng’a iseitani omoirete.*”

Taf: “... *mtu asidanganye kuwa kulikuwa na jambo au ni fulani alimroga ama kama ungeenda mahali ungemponya, jua ni shetani alimchukua.*”

Katika mfano ulionukuliwa hapo juu, mhutubu alimwonya mjane dhidi ya kufikiria kuwa kifo cha mumewe kilikuwa kimesababishwa na vianzo vingine kama ilivyodhihirika kupitia kwa kauli “**onde takong’aina ng’a eke ikiarengo**”-*mtu asikudanganye kuwa kulikuwana jambo*. Katika kauli hii, pengine mhutubu alimaanisha kuwa mjane asiambiwe kuwa mumewe alikuwa na ugonjwa wa sinaa uliosababisha kifo chake. Alimwonya pia dhidi ya kufikiria kuwa iwapo angeenda mahali pengine isipokuwa hospitali, mumewe angepona kama ilivyobainika kupitia kwa kauli “**onye gwachiete aande konang’a ikwamobwenetie**”- *kama ungeenda mahali ungemponya*. Mjane alikuwa na haki ya kujua chanzo cha kifo cha mumewe kwa sababu alikuwa mpenzi wake. Aidha alikuwa na uhuru wa kujiliwaza kutokana na kifo cha mumewe hata kama hangetulizwa. Kulikuwa na uwezekano kuwa mjane hangeafiki kuonywa dhidi ya kifo cha mumewe lakini mhutubu alipomwonya hadharani bila hiari yake, aliutishia uso hasi wa mjane huyo kwa kuingilia uhuru wake. Aidha, mhutubu alimwonya mjane huyo dhidi ya kudanganyika kuwa kifo cha mumewe kilikuwa kimesababishwa na uchawi au mtu fulani. Alimwonya na kumwambia kuwa ilikuwa vyema aamini kuwa shetani

ndiye aliyesababisha kifo cha mumewe lakini kwa vyovyote vile ajue kuwa Mungu alikuwa na uwezo. Tazama mfano wa usemi ufuatao:

EkG: “*Monto onde takong’aina nga nyarebe omoitete gose omorogete, manya nga isetani oirete, nyasaye nabwate okobua.*”

Taf: “*Mtu yeyote asikudanganye kuwa ni fulani alimroga au aliyemuua, jua kuwa ni shetani alimchukua, Mungu ana uwezo.*”

Katika mfano huo, kauli “**monto onde takong’aina ng’a inyarebe omoitete gose omorogete**”- mtu yeyote asikudanganye kuwa ni fulani alimroga au alimuua ilimwonya mjane dhidi ya kufikiria kuwa kifo cha mumewe kilikuwa kimesababishwa na mtu kupitia uchawi. Kawaida, kifo kinapotokea ghafla watu hushangaa na hutaka kufahamu kilichosababisha kifo hicho. Vile vile mtu anapougua kwa muda mrefu, watu hataka kujua mtu huyo ameugua ugonjwa upi. Kutokana na rambirambi hiyo, mjane hakutarajiwa ajue chanzo cha kifo cha mumewe wala kufahamu ukweli kuhusu ugonjwa wake. Kwa mujibu wa Yule (1996), kumuonya mtu kunamnyima uhuru wa kutenda atakavyo na hivyo matamanio ya uso wake hasi yanaingiliwa. Mhutu alipomwonya mjane hivyo, alimnyima nafasi ya kujua ukweli kuhusu ugonjwa na kifo cha mumewe au mjane alikosa uhuru wa kufanya atakavyo. Aidha, inawezekana kuwa mjane lionywa bila hiari yake na hivyo uso wake hasi uliingiliwa.

6:2:4 Kumtolea msikilizaji ushauri

Ushauri ni maoni yanayotolewa kwa mtu ili yamsaidie kupata suluhisho fulani au kufanya jambo fulani. Katika mazungumzo, mzungumzaji anaweza kumshauri msikilizaji kuhusu jambo, hali au kitu fulani. Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa ushauri unaweza kutokea bila idhini ya msikilizaji na unapotokea hivi, huwa kitishio kwa uso hasi wa msikilizaji huyo. Wanaendelea kueleza kuwa kila mwanadanu hupenda kuwa na uhuru na haki katika maisha yake ambapo hapendi kuingiliwa kwa vyovyote bila kibali chake. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane, wahutu walitishia uso hasi wa wajane walipowatolea ushauri kuhusu hali za maisha na mambo mbalimbali. Mifano ifuatayo inadhihirisha hayo: Wakati **MH7** alikuwa akitoa rambirambi kwa mjane **B**(mwanamume), alitishia uso hasi wa mjane huyo aliposhauri kuwa aendelee kumwamini Mungu ingawa mkewe alikuwa ameaga . Mfano ufuatao unadhihirisha hayo:

EkG :“... *omenye ase enyomba ya tata amatuko onsi yo obogima bwao.*”

Taf: “... *uishi nyumbani mwa Mungu siku zote za maisha yako.*”

Katika mfano huo, mhutu alimshauri mjane kuwa aendelee kumwamini na kumtumikia Mungu siku zote za maisha yake. Hilo lilibainika kupitia kauli “**omenye ase enyomba ya tata amatuko onsi yo obogima bwago**”- uishi nyumbani mwa Mungu siku zote za maisha yako. Mhutu alimaanisha kuwa mjane asiache wokovu wake bali imani yake kwa Mungu iweze kukomaa kila wakati. Vile vile alimaanisha kuwa mjane amtukuze na kumwabudu Mungu hadharani huku akitenda mema na haki kwa wote na matendo hayo yaweze kupendwa na kuigwa na wengi. Inawezekana kuwa ushauri huo ulitolewa bila idhini ya mjane. Mjane

alipojipata katika hali geni ya maisha kwa sababu ya kifo cha mkewe, alikuwa na uhuru wa kuamua namna angeishi maisha hayo mapya pamoja na watoto wake. Angeweza kuendelea kumtumikia Mungu au angekoma na imani yake iffie. Mhutubu alipomtolea mjane ushauri huo, aliingilia uhuru wake kwa kumnyima uwezo wa kufanya alivyotaka na kuishi apendavyo. Mifano mingine ambapo mhutubu huyo alimtolea mjane **B** ushauri ilikuwa pale ambapo alimwambia kuwa aweke tumaini lake kwa Mungu kwa sababu ndiye angemsaidia. Alimwambia pia ashikirie wokovu wake na aendelee kutenda mema kwa watu. Rambirambi zifuatazo zinadhihirisha hayo.

EkG: "Ogokonya kwago nigo korarwe ase omonene, **mosemerie chingaki chionsi na oimokie egekombe kio ogotoreka.**"

Taf: "usaidizi wako utatoka kwa Mungu, mtumainie nyakati zote na ukibebe kikombe cha wokovu."

EkG: "Imokereria Nyasae igoro ase amaiso ya abanto abange."

Taf: "Mtukuze Mungu hadharani mbele ya macho ya watu wengi."

Katika mifano iliyonukuliwa hapo juu, mhutubu alimshauri mjane **B** aendelee kumtumainia Mungu nyakati zote zikiwemo nyakati hizo za huzuni alizokuwa amefiwa. Hilo lilidhihirika kupitia kauli "**mosemerie chingaki chionsi**"- mtumainie nyakati zote." Alimshauri na kumhimiza aendelee na wokovu wake kama ilivyobainika kupitia kauli "**oimokie egekombe kio ogotoreka**"- ukibebe kikombe cha wokovu." Aidha, alimshauri asiogope kutangaza habari za Mungu kwa watu wote kama ilivyodhihirika kupitia kauli "**imokereria Nyasae igoro ase amaiso ya abanto abange**"- mtukuze Mungu hadharani mbele ya macho ya watu wengi. Ushauri huo ulimtaka mjane atende alivyotaka mhutubu. Kwa upande mwingine, mjane alikuwa na uhuru wa kutenda alivyopenda baada ya kifo cha mkewe na hivyo ushauri wa mhutubu huenda uliathiri uso hasi wa mjane huyo iwapo ulikuwa umetolewa bila hiari yake. Rambirambi za **MH9** kwa mjane **B** zilitishia uso hasi wa mjane huyo alipomtolea ushauri kuwa aende nyumbani kwake wajuane ili aweze kumsaidia. Alisema:

EkG: "Inchwe inka tororane naye nabo togosanga amo."

Taf: "Uje pale nyumbani tufahamiane, tutashirikiana pamoja."

Katika mfano huo, mhutubu alimpa mjane ushauri kuwa aenda kwake kama ilivyodhihirika kupitia kauli "**inchwe inka tororane naye nabo togosanga amo**"- uje pale nyumbani tufahamiane, tutashirikiana pamoja. Mjane alikuwa na uhuru wa kuamua kufanya chochote, angeweza kukataa ushauri huo kwa sababu kulikuwa na uwezekano hangetaka kuingiliwa. Mhutubu alipomtolea ushauri huo alimnyima nafasi ya kufanya alivyotaka. Hivyo, aliutishia uso wake hasi. **MH16** alitishia uso hasi wa mjane **C** (mwanamke) alipomshauri kuwa, adumu kanisani kwa sababu angewapta akina mama waliokomaa ambao wangemshauri namna ya kuishi maisha ya ujane. Ushauri huo huenda ulikuwa kinyume na matamanio ya mjane huyo na hivyo ulitishia uso wake hasi. Mfano ufuatao unadhihirisha hayo:

EkG: “*Omong’ina omenye ekanisa, otamere aroro egere onyore abang’ina baria baberire ekanisa bakong’ire ekiagera konyara bare kobabeke buya ababoraka.*”

Taf: “*Mama uishi kanisani, ukimbilie pale ili upate akina mama wale wamekaa kanisani wamekomaa kwa kuwa wanaweza kuwashauri wajane.*”

Katika mfano huo, mhutubu alimtaka mjane aendelee na kazi ya Mungu, aendelee kumtumainia Mungu nyakati sote. Aidha, mhutubu alimshauri mjane asiweze kukosa kanisani kwa sababu angewapata akina mama waliokuwa wamekomaa wamshauri jinsi angeishi maisha mapya ya ujane. Hili lilikuwa dhahiri kupitia kauli *mama uishi kanisani, ukimbilie pale ili upate akina mama wale wamekomaa*. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), ushauri hutishia uso hasi wa msikilizaji kwa kuingilia uhuru wake wa kutaka kuwa huru na wakati unatolewa bila idhini. Mjane alipofiwa, alihitaji uhuru wa kujiamulia mambo mbalimbali kuhusu maisha yake. Angeweza kuamua kuendelea kushiriki katika kanisa hilo alilokuwa akishiriki hapo awali kabla ya kifo cha mumewe au angebadilisha kanisa. Aidha, kulikuwa na uwezekano mjane aache kuenda kanisani kwa kuhofia kuingiliwa na akina mama hao waliokuwa wanawashauri wajane. Vile vile huenda ushauri huo ulitolewa kwa mjane bila idhini yake na hivyo uliingilia uhuru wake. Aidha, **MH30** alitishia uso hasi wa mjane **E**(mwanamke) alipomtolea ushauri kuwa awe akiishi kwa amani pamoja na watoto wake ili waweze kuepuka magonjwa yanayosababishwa na msongo wa mawazo. Alipotoa rambirambi alisema:

EkG: “*... timoba ne chinkwana chio ogotogonyerana amo na abana. Makueri tatageti igo ase eng’encho nigo orarengererie naende ebirengererio ebio birete amarwaire.*”

Tafsiri: “*... msije mkawa na mazungumzo ya mabishano na watoto wako. Kifo hakitaki hivyo kwa sababu utafikiria na fikira hizo zitaleta magonjwa.*”

Katika mfano huo, mhutubu alimshauri mjane kuwa aelewane na watoto wake na wawe na mazungumzo yanayoleta amani. Aliwashauri wasiwe na mazungumzo ya kutopatana kwa kuwa mzozo baina yake na watoto ungemletea msongo wa mawazo ambao ungeleta magonjwa. Hivyo, aliwashauri waweze kuepukana na mzozo wowote ambao ungeleta ugomvi au mabishano kwa sababu mumewe alikuwa amekwisha aga. Kwa upande mwingine, mjane alikuwa na haki ya kutaka kubaki huru bila kuingiliwa kwa vyovyote vile au kupewa ushauri wowote. Huenda pia mjane hakutaka kushauriwa vile kwa sababu huenda aliwaelewa watoto wake na alijua ni namna gani angetangamana nao. Alipopewa ushauri huo bila hiari yake, uso wake hasi ulitishiwa.

6:2:5 Kumkumbusha msikilizaji kuhusu jambo au hali fulani

Kulingana na Brown na Levinson (1987), kuna taarifa ambazo hutishia nyuso za wasikilizaji wakati zinarejelewa bila idhini au kwa sababu ya matokeo mabaya yanayotokana na taarifa hizo. Wakati mzungumzaji anamkumbusha msikilizaji kuhusu hali au mambo yanayomhusu bila idhini yake, huwa anatishia uso hasi wa msikilizaji huyo. Hii ni kwa sababu huenda msikilizaji asihitaji kukumbushwa kuhusu chochote katika maisha yake au mzungumzaji

anaweza kumkumbusha hali mbaya ambayo inaweza kumkera msikilizaji. Katika utoaji wa rambirambi kwa wajane, kuna wakati wahutubu walijipata wamewakumbusha wajane kuhusu hali au mambo mbalimbali katika maisha yao na kutishia uso hasi wa wajane hao. Mifano ifuatayo inadhihirisha hayo: Vitendo vya kutishia uso hasi vilidhihirika katika rambirambi za **MH2** kwa mjane **A**(mwanamume). Vitendo hivyo vilitokea wakati mhutubu alimkumbusha mjane kuwa alifaa awe mwombezi kwa sababu maombi ndiyo yangempa motisha wa kuishi. Hili lilidhihirika katika rambirambi ifuatayo:

EkG: “Buna mwarenge gosaba more amo, ogenderere **Amasabo naro aragokonye**, yatakupa motisha wa kuishi.”

Taf: “Mlivyokuwa mkiomba pamoja, uendele. Maombi ndiyo yatakusaidia, yatakupa motisha wa kuishi.”

Katika rambirambi hiyo, mhutubu alimkumbusha mjane jinsi walikuwa wakiomba wakati walikuwa pamoja na mkewe. Alimkumbusha aendele kuomba kama ilivyodhihirika katika kauli “**amasabo naro aragokonye**”- maombi ndiyo yatakusaidia. Kulingana na mhutubu, maombi yangemwelekeza na kumsaidia mjane katika maisha yake. Kutokana na rambirambi, kulikuwa na uwezekano kuwa mhutubu alimkumbusha mjane bila idhini yake. Kwa upande mwingine, mjane alikuwa na uhuru wake wa kufanya alivyotaka na pia kuamua namna angeishi, kumkumbusha kuhusu maombi kuliingilia uhuru wake. Hii ni kwa sababu mjane alinyimwa nafasi ya kujiamulia kile angefanya au huenda hakutaka akumbushwe hivyo. Mhutubu basi aliingilia uso hasi wa mjane huyo alipofanya hivyo. Mfano mwingine ambapo mhutubu huyo alimkumbusha mjane **A**, ni pale ambapo alimwambia kuwa amebaki kuendeleza maisha yake, ya watoto wake na hata wajukuu. Alisema:

Kisw: “Mzee umebaki kuendeleza maisha yako, ya watoto wako na wajukuu. Kama ulivyonilelea mikaile tulikuwa tukiishi pamoja, nina imani utafanya hivyo”

Katika mfano huo, mhutubu alimkumbusha mjane kuwa hakukuwa na jambo lingine la kufanya bali ilikuwa kuwalinda, kuwalekeza na kuwawajibikia watoto wake na hata wajukuu. Aidha, alimkumbusha kuhusu maisha waliyokuwa wakiishi hapo awali wakati mjane alikuwa akiishi kwake na wakati huo mjane alikuwa kijana hakuwa ameo. Mhutubu alimkumbusha jinsi alimlelea watoto wake vyema na kumwambia kuwa alikuwa na imani kuwa angeweza kuwalea watoto pamoja na wajukuu waliokuwa wameachwa baada ya mkewe kuaga. Pengine mjane hakutaka kukumbushwa kuhusu maisha yake ya zamani au huenda hakutaka watu wajue kuwa alikuwa akiishi kwa msamaria mwema ambaye hakuhusiana naye au hakukuwa na uhusiano wa kiukoo. Mhutubu alipomkumbusha hivyo bila idhini yake, kulikuwa na uwezekano kuwa aliingilia uhuru wake wa kutotaka kukumbushwa kuhusu maisha hayo ya zamani pamoja na maisha mapya ya ujane au uhuru wake wa kutotaka kukumbushwa hadharani uliingiliwa.

Kulikuwa na uwezekano kuwa **MH8** alipomkumbusha mjane **B**(mwanamume) kuhusu majukumu ambayo angetekeleza baada ya mkewe kuaga alitishia uso hasi wa mjane

huyo. Naye **MH15** akitoa rambirambi zake kwa mjane **C**(mwanamke) kuhusu majukumu hayo aliingilia uso hasi wa mjane huyo. Katika rambirambi zake alisema:

EkG: “Konye nigo obwate egasi eyemo korende **bono gwatigaire na amajukumu abere** yo okoba buna omokungu naende obe buna omosacha.”

Taf: “Ulikuwa na jukumu moja lakini sasa umekuwa na majukumu mawili; ya kuwa kama mama na baba.”

EkG: “**Omanye kwabekire chianga ibere, kwabekire eyanga yo omogaka ogo amo na eyago.**”

Taf: “Ufahamu umevalia nguo mbili, ya mumewe na yako.”

Katika mfano wa kwanza, kauli “**bono gwatigaire na amajukumu abere**”- sasa umekuwa na majukumu mawili ilimkumbusha mjane **B** kuwa kazi ambayo angefanya ingeongezeka. Angetekeleza majukumu yake kama mume na yale yaliyotekelezwa na marehemu mkewe. Katika mfano wa pili, mjane **C** angetekeleza majukumu yake na yale yaliyotekelezwa na mumewe alipokuwa hai kama ilivyobainika katika kauli *ufahamu umevalia nguo mbili, ya mumewe na yako*. Kauli hizo zilimkumbusha wajitahidi na wajikaze sana zaidi ya vile walikuwa wakifanya ili waweze kuyakamilisha majukumu hayo yote. Ujumbe huo uliweza kutishia uso hasi wa wajane hao iwapo hawakutaka wakumbushwe kuhusu majukumu hayo. Rambirambi za **MH16** na **MH18** kwa mjane **C**(mwanamke) zilidhihirisha vitendo vilivyotishia uso hasi wa mjane huyo. Mifano ya rambirambi ifuatayo inabainisha hayo:

EkG: “**Konye nigo ogotobia abande buna amakweri na amakoro, korende ekeri riakonyorire nigo rikoba egento kiogokumia.**”

Taf: “Umekuwa ukiwaambia wengine kuwa kifo ni cha zamani, lakini wakati kimekupata kinashangaza.”

EkG: “... **kera omento nabwate etiketi yaye omoguko ekeri eraike there is no question you just leave so pole sana.**”

Taf: “... kila mtu ana tiketi yake mfukoni wakati itawadia atakufa tu, kwa hivyo pole sana.”

Katika mfano wa kwanza, **MH16** alimkumbusha mjane kuwa hata yeye alikuwa akiyahudhuria mazishi ya wengine na kuwafariji, hivyo naye alifaa afarijike kwa kukumbwa na msiba huo. Katika mfano wa pili, **MH18** naye alimkumbusha mjane huyo kuwa kila mtu angekufa wakati wake ungefika. Alimkumbusha kuwa ilikuwa vigumu kuzuia kifo na hakuna aliyejua angekufa lini. Katika mfano hiyo, wahutubu walimkumbusha mjane kuhusu hali mbaya ya kifo ambayo huenda hakutaka akumbushwe kwa kuwa mumewe alikuwa ameaga na kumwacha katika hali ya huzuni. Aidha, mjane alikuwa na haki ya kubaki huru asiingiliwe kwa kukumbushwa chochote kuhusu kifo. Wahutubu walipomwingilia hivyo bila hiari yake, bila shaka walitishia uso hasi wa mjane huyo. Rambirambi za **MH20** na **MH22** kwa mjane **D**(mwanamume) zilitishia uso hasi wa mjane huyo walipomkumbusha kuhusu kifo cha mkewe. Katika rambirambi zao walisema:

EkG: “*Ogokwa kwarengeo korwa kare, ogoku okoiga kawaida... ekeru gwatokeire iga, goika toiche amo toenane pole.*”

Taf: “*Kifo kilikuwepo tangu zamani, kifo hiki ni kawaida... kinapotokea hivyo lazima tuje pamoja tufarijiane.*”

EkG: “*Toba no obwoba ekiagera egasi omorugi oo aetwe yaerire naende manya inga ogokora kwaye komotunyane ekeru yeso akoirania oboruoti bwaye.*”

Taf: “*Usiwe na woga kwa sababu kazi aliyopewa mkewe imekamilika tena fahamu kuwa matendo yake yatamfuata wakati Yesu atarudisha ufalme wake.*”

Katika mfano wa kwanza, **MH20** alimkumbusha mjane kuwa kifo kilikuwa cha zamani na hivyo watu hawakufaa kuogopa kwa sababu kingewaleta watu pamoja. Aidha, alikichukulia kifo cha mke wa mjane **D** kuwa cha kawaida ambacho hakikufaa kumfanya mjane **D** aogope. Hili lilidhihirika kupitia kwa kauli “**ogokwa kwarengeo korwa kare, ogoku okoiga kawaida**”- *kifo kilikuwepo tangu zamani, kifo hiki ni kawaida*. Katika mfano wa pili, **MH22** alimkumbusha mjane kuwa asiwe na woga kwa sababu mkewe alikufa kwa kuwa alikuwa amekamilisha kazi aliyokuwa amepewa na Mungu na matendo yake yangemfuata. Wakati wa msiba, aliyefiwa huwa na matamaniao ya kufarijiwa na kuliwazwa. Katika rambirambi hizo, wahutubu walienda kinyume na matarajio ya mjane huyo kwa kumkumbusha kuwa kifo cha mkewe hakikufaa kumwogopesha kwa sababu walidai kuwa kifo kilikuwa cha kawaida na mkewe alikuwa amekamilisha maisha aliyokuwa amepewa na Mungu. Kumkumbusha mtu kuhusu jambo mbaya katika maisha yake na bila idhini yake, kunatishia uso hasi wa mtu huyo (Brown na Levinson, 1987; Yule, 1996). Wahutubu hao walipomkumbusha mjane kuhusu kifo cha mke wake, bila shaka walitishia uso hasi wa mjane huyo. **MH31** na **MH34** walitishia uso hasi wa mjane **F**(mwanamke) walipokuwa wakitoa rambirambi zao. Mifano ifuatayo inadhihirisha hayo.

EkG: “*... imoisonde kwarwa gotuguta mosubati omino naende aya akonyorire, pole sana*”

Taf: “*... ni juzi ulimzika dadako tena haya yamekupata, pole sana.*”

EkG: “*... bono naye gwatigaire, omogaka oo ochire, bono kong’a naende abana aba bago bakobwatesi.*”

Taf: “*... sasa ni wewe umebaki, mume wako ameaga, kuwa mjasiri sasa tena hawa watoto wako wakusaidie.*”

Katika mfano wa kwanza, **MH31** alimkumbusha mjane kuhusu kifo cha dadake kilichokuwa kimetokea siku chache zilizokuwa zimepita huku kikifuatwa na kifo cha mumewe. Hilo lilidhihirika kupitia kwa kauli “**imoisonde kwarwa gotuguta mosubati omino naende aya akonyorire**”- *ni juzi ulitoka kumzika dadako tena haya yamekupata*. Habari hiyo ilikuwa mbaya kwa vile ilikuwa inahusu kifo na ilimtonesha mjane kidonda cha upweke kilichokuwa kimesababishwa na kifo cha dadake. Kabla ya kidonda hicho kupona mumewe pia alifariki na mhutubu alimkumbusha hivyo. Mjane huenda hakutaka kukumbushwa kuhusu hali hiyo

ya kihoro kwa vile ilimsababishia huzuni moyoni. Katika mfano wa pili, **MH34** alimkumbusha mjane kuhusu hali yake ya upweke iliyokuwa imesababishwana kifo cha mumewe na namna ingemfaa awe jasiri akiwa katika hali hiyo ya ujane. Kulikuwa na uwezekano kuwa wahutubu hao walimkumbusha mjane habari. Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha vitendo vilivyotishia uso hasi wa wajane wakati wahutubu walikuwa wakitoa rambirambi zao katika muktadha wa mazishi. Aidha, jedwali linaonyesha idadi ya wahutubu waliotumia vitendo hivyo.

Jedwali 6:2(b): Muhtasari wa vitendo vilivyotishia uso hasi wa wajane na idadi ya watumizi.

Uso hasi	Vitendo vilivyotishia uso hasi	Idadi ya watumizi
	<ul style="list-style-type: none"> • Kuamrisha na kutoa ombi kwa msikilizaji 	7
	<ul style="list-style-type: none"> • Kumtolea msikilizaji maagizo 	8
	<ul style="list-style-type: none"> • Kuonya msikilizaji 	4
	<ul style="list-style-type: none"> • Kumtolea msikilizaji ushauri 	4
	<ul style="list-style-type: none"> • Kumkumbusha msikilizaji kuhusu jambo au hali fulani 	9
	Jumla	32
	Sampuli	36
	Asilimia	88.89

Jedwali la 6 Muhtasari wa uhakiki wa vitendo vya wahutubu vilivyotishia nyuso za wajane katika rambirambi za mazishi

Nyuso zilizotishiwa	Vitendo vya kutishia	Idadi ya watumizi
1. Uso chanya	<ul style="list-style-type: none"> • Kumdunisha msikilizaji 	2
	<ul style="list-style-type: none"> • Kumtusi msikilizaji 	2
	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa malalmishi kwa msikilizaji 	2
	<ul style="list-style-type: none"> • Kuzungumzia mambo kuhusu maisha ya msikilizaji 	4
	Jumla	10
	Sampuli	36
	Asilimia	27.78

2. Uso hasi	• Kuamrisha na kutoa ombi kwa msikilizaji	7
	• Kumtolea msikilizaji maagizo	8
	• Kuonya msikilizaji	8
	• Kumtolea msikilizaji ushauri	4
	• Kumkumbusha msikilizaji kuhusu jambo au hali fulani	4
	Jumla	32
Sampuli	36	
Asilimia	88.89	

7: MATOKEO YA UTAFITI

Lengo la utafiti lilikuwa kuhakiki vitendo vya wahutubu ambavyo vilitishia nyuso za wajane katika rambirambi za mazishi. Kwa mujibu wa lengo hili, utafiti uligundua kuwa wahutubu walipotoa rambirambi kwa wajane, ilikuwa vigumu kwao kuepuka kutenda vitendo vya usemi ambavyo vingetishia nyuso za wajane. Vitendo hivyo vilitokea wakati ambapo wahutubu walitoa kauli ambazo ziliingiliana na kukinzana na matamano ya wajane, hali iliyosababisha kuibuka kwa hisia za aibu kwa wajane au kuwalazimisha wajane kufanya mambo kinyume na matarajio yao. Wahutubu walipotoa kauli hizo, bila shaka waliingilia na kuathiri aidha uso chanya wa wajane au uso hasi.

Kuna vitendo vya usemi ambavyo wahutubu walitekeleza na kuathiri uso chanya wa wasikilizaji ambao walikuwa wajane. Vitendo hivyo vilikuwa kama vile kumdunisha msikilizaji, kumtusi au kumsimanga msikilizaji, kutoa malalamishi kwa msikilizaji na kuzungumzia mambo kuhusu maisha ya msikilizaji kwa namna iliyokuwa haikubaliki. Katika uhakiki wa vitendo hivyo, utafiti uligundua kuwa wahutubu wengi katika eneo bunge la Bobasi, waliathiri sana uso chanya wa wajane wakati walikuwa wakizungumzia kuhusu maisha ya wajane bila kibali kutoka kwa wajane hao. Kitendo hicho kilikuwa na watumizi 4 huku vitendo vingine vya kumdunisha, kumtusi na kutoa malalamishi kwa msikilizaji vilitumiwa kwa viwango sawa ambapo vilikuwa na watumizi wawili kwa kila kimoja.

Aidha, wahutubu walitekeleza vitendo vya usemi ambavyo viliathiri nyuso hasi za wajane. Vitendo hivyo vilikuwa kama vile kuamrisha na kutoa ombi kwa msikilizaji, kumtolea msikilizaji maagizo, kuonya msikilizaji, kumtolea msikilizaji ushauri na kumkumbusha msikilizaji kuhusu jambo, hali au fulani. Katika vitendo hivyo, utafiti uligundua kuwa wahutubu walitekeleza sana vitendo vya kuwakumbusha wajane kuhusu mambo fulani katika maisha yao. Vitendo hivyo vilikuwa na watumizi 9 vikifuatwa na vya kuwatolea maagizo vikiwa na watumizi 8 na vya kuamrisha na kutoa ombi vilikuwa na watumizi 7. Vitendo vya kuwaonya na kuwatolea wajane ushauri vilikuwa na matumizi machache ya watumizi 4 kwa kila moja.

Utafiti huu uligundua kuwa hata ingawa wahutubu walijaribu kuviepuka vitendo vilivyotishia nyuso za wajane, ilikuwa vigumu na hivyo walijipata wamevitenda kupitia kwa usemi wao. Aidha, utafiti uligundua kuwa wahutubu walitekeleza sana vitendo vilivyotishia

uso hasi wa wajane ambavyo vilitekelezwa kwa asilimia 88.89 kuliko vile vilivyotishia uso chanya vilivyotekelezwa kwa asilimia 27.78.

8: Hitimisho

Hitimisho kuu katika utafiti huu ni kuwa lugha ya upole katika utoaji wa rambirambi kwa wajane ina jukumu kubwa katika udumishaji wa heshima za kihisia, uimarishaji wa mahusiano, ujenzi wa ujasiri na kuyafanya maombolezo kuendelezwa bila utata. Wahutubu walidhihirisha matumizi ya lugha ya upole katika kuyahifadhi na kuyakidhi mahitaji ya nyuso za wajane kupitia kwa uteuzi wa mikakati mbalimbali ya upole iliyodumisha nyuso hizo. Kadhalika, ni wazi kuwa ilikuwa vigumu kuviepuka vitendo vilivyotishia nyuso za wasikilizaji wakati wa mazungumzo kwani wahutubu waliweza kutishia nyuso za wajane wakati wa kutoa rambirambi. Katika hali hiyo, wahutubu walipunguza vitendo hivyo vilivyotishia kupitia kwa uteuzi wa mikakati faafu. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ni haki pia kuhitimisha kuwa japo wahutubu wa jamii ya AbaGusii wanazingatia lugha ya upole wanapotoa rambirambi zao kwa wajane, ni nadra kuviepuka vitendo vya kutishia nyuso katika maingiliano ya kila siku au katika mazungumzo yoyote.

9: Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, yafuatayo yanapendekezwa:

1. Madahii inaweza kuendelezwa kwa kuchunguza mikakati inayotumiwa na wahutubu kupunguza vitendo vinavyotishia nyuso zao wakati wanapotoa rambirambi kwa wajane katika eneo hili la Bobasi. Utafiti huu pia unaweza kuendelezwa kwa kuzingatia mitazamo tofauti ya upole kama vile mtazamo wa Lakoff kuhusu upole au Leech.
2. Utafiti unaweza kufanywa ili kutathmini upole katika rambirambi kwa wajane katika lugha zingine za kiafrika ili kuleta maridhiano namna wanajamii wa lugha tofauti tofauti hudhihirisha upole wakati wa utoaji rambirambi.
3. Utafiti unaweza kufanywa ili kulinganisha kiasi cha upole katika rambirambi za mazishi kwa wajane wa kiume na wa kike katika jamii ya AbaGusii na jamii zingine za Kiafrika.
4. Kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika rambirambi za wahutubu kwa wajane pekee katika eneo bunge la Bobasi, utafiti mwingine unaweza kufanywa kutathmini namna wahutubu wanadhihirisha upole kwa aliyeaga wakati wa kutoa rambirambi zao.

Funding: This research received neither internal nor external funding

Shukurani (Acknowledgments)

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na siha njema nilipokuwa nikifanya kazi hii. Neema na fadhili zake zisizokadirika zimeniwezesha kukamilisha kazi hii. Shukurani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Eucabeth Mongare na Dkt. Francis Kariithi kwa kujitolea kwa moyo wenu wote kunishauri na kunielekeza kwa njia zote. Mliitwaa kazi hii, mkaisoma na kuidurusu bila kuchoka ili kuhakikisha ufanisi wa kazi hii. Bila msaada wenu singekuwa mahali nilipo sasa. Mungu awaneemeshe na kuwajalia siku zote. Shukurani za kipekee kwa dadangu Janes kwa ufadhili wako na himizo ulilonipa lilinipa ari ya kuendelea kusoma. Isitoshe, shukurani za dhati kwa babangu James na mamangu Yuniah kwa kuniombea na kunihimiza nikaze mwendo. Sitawasahau ndugu zangu Peter na Dennis kwa upendo mlionyesha kwangu na msaada wenu ulinifaa sana. Mwisho ningependa kuwashukuru wote walionifaa kwa njia moja au nyingine ambao sikuweza kuwataja, Mungu awabariki.

Conflict of interest: There was no conflict of interest declared by the author.

Disclaimer statement

This work is part of a thesis submitted to Kisii University for award of Masters Degree in Kiswahili.

Author bionate

Nyabuto Judy Nyaboke is a student in Kisii University persuing Masters in Kiswahili in the department of Languages, linguistics and literature. She is a trained teacher where she obtained her degree in Bachelors in Education Arts (kisw/ hist) from Kisii university. Her research interest is on politeness and how people ambrace polite or impolite language in their day to day activities in different contexts of life.

Authorship and level of contribution

My supervisors Dr. Francis Kariithi and Dr. Eucabeth Mong'are advised and guided me in every way; they took the work read it and reviewed it tirelessly to ensure the success of this work.

Marejeleo

- Akama, J. S. & Maxon, R. (2006). *Ethnography of the Gusii of Western Kenya. A vanishing cultural heritage*. New York: The Edwin Mellen Press, 293-316.
- Billows, F. R., & Krauss, R. M. (1988). Dominance and accommodation in the conversational behavior of same and mixed gender dyads. *Language and communication*, 8, 183-194.
- Bloor, M., & Bloor, T. (2007). *The Practice of critical discourse analysis: An introduction* London: Hodder Arnold Press.
- Brown, P., & Levinson, S. (1978). *Politeness! Some universal in language usage*, 62-135. Cambridge University Press.
- Brown, P., & Levinson, S. (1987). *Universals in language use: Politeness phenomena*. Katika, E. N Goody (ed.) *Questions and politeness in social interaction*, 56-311. Cambridge University Press.
- Buliba, A., Njogu, K., & Mwihaki, A. (2006). *Isimujamii kwa wanafunzi wa Kiswahili*. Kur. 60. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Calhoun, C. J. (2002). *Dictionary of the social sciences*. New York: Oxford University Press.
- Calhoun, C. J. (2002). *Research methodologies for the creative arts and humanities: Participant observation research*. New York: Oxford University Press.
- Cambridge (2008) *Advanced learner's dictionary* (3rd edition). Cambridge University Press.
- Capone, A. (2010). On progmemes again: Dealing with death. *La Linguistique*, (46). 3-21.
- Chidimma, M.E. & Mmadike, B.I. (2016). Speech act analysis of Igbo utterances in funeral rites. *Ogiris: Anew Journal of African Studies*, (12), 2016.
- Clark, Robert E. & Emily E. LaBeff. (1982). Death telling: Managing the delivery of bad news. *Journal of Health and Social Behaviour* 23(4), 366-380.
- Coates, J. (1993). *Women, men and language*. London: Longman.
- Cresswell, J. W. (2009). *Research design: Qualitative, quantitative and mixed methods approaches* 3rd edition, kur.52, Los Angeles, CA: Sage.
- Creswell, J. W & Miller, D. L. (2000). Determining validity in qualitative inquiry. *Theory into practice*, 39(3), kur 124-132.
- Creswell, J. W. (2012). *Qualitative inquiry and research design: Choosing among the five traditions* (3rd edition). Thousand Oaks, CA: Sage.
- DeWalt, K. M., & DeWalt, B. R. (2002). *Participant observation: A guide for fieldworkers*. Walnut Creek, CA: AltaMira Press.
- Ezeifeke, C & Ogbazi, I. (2014). Your're responsible for his death: Widowhood in Igbo gender construction and struggle for agency in selected literary texts. *International Journal of Language and Literature*, 2(3), 115-133.
- Fairclough, N. (2001a). Critical discourse analysis as a method in social scientific research. Katika R. Wodak & M. Meyer (Whr.), *Methods of critical discourse analysis*. London: Sage.
- Fromkin, V. na Rodman, R. (1998). *Introduction to languages*, (6th edition). California, Harcourt Brace College Publishers.
- Gatambuki, M.G (2010). A cognitive linguistic analysis of Gikuyu euphemism. *Tasnifu ya*

shahada ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

- Gay, L.R. (1992). *Educational research: Competencies for analysis and application* (3rd edition). Paris: Meril Publishing Company.
- Goffman, E. (1959). *The presentation of self in everyday life*. New York: Anchor Books.
- Goffman, E. (1967). On face work: An analysis of ritual elements in social interaction. Katika: E. Goffman, *Interaction ritual: Essays on face-to-face behavior*, kur. 5-46. New York: Anchor Books.
- Grice, H.P. (1975). *Logic and conversations*. Katika Peter Cole & Jerry Morgan (eds.) *Syntax and semantics*. New York, N.Y: Academic Press.
- Habwe, J. H. (2010). Dialogue drama in Kenyan political speeches and its pragmatics implications. Kenya: University of Nairobi. *Nordic Journal of African Studies* 19(3): pp 165-180.
- Habwe, J. H. (2010). Politeness phenomena: A case of Kiswahili honorifics. Kenya: University of Nairobi. *Swahili forum*, 17, 126- 142.
- Halliday, M.A.K. (2003). "On the 'architecture' of human language." Katika *On language and linguistics*. Volume 3 in the collected works of M.A.K. Halliday, kur 1. London and New York: Equinox.
- Harry, H. (1954). *Language in culture: Conference on the inter-relations of language and other aspects of culture*, 31(118): 281-282. University of Chicago Press.
- Haug, Y. (2007). *Pragmatics*. New York, NY: Oxford University Press.
- Hill, B., Sachiko, I., & Akiko, K. (1986). *Universals of linguistic politeness. Quantitative evidence from Japanese and American English. Journal of pragmatics*, 10 pp, 62, 347-371
- Hobbs, P. (2003). The Medium is the message: Politeness strategies in men's and women's voice mail message. *Journal of Pragmatics*, (35), 243-262.
- Hymes, D. (1964). *A Language, culture and society*. New York & London: Harper and Row, 1964, 34. Cambridge University Press.
- Josselson, R. (2007). The ethical attitude in narrative research: Principles and practicalities. Katika: D. J. Clandinin (Mh.), *Handbook of narrative inquiry*, Kur. 537-566. Thousand Oaks, CA: Sage.
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la pili* (2007). Oxford University Press, Kenya.
- Kariithi, F. (2010). Mikakati ya upole katika matumizi ya lugha ya vijana. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Imetolewa kwa <http://erepository.uonbi.ac.ke:8080/handle>
- Kenya National Bureau of Statistics, (2009). *Kenya Population and Housing Census; Population and household distribution by socio-economic characteristics*. Volume II.
- Kinyua, G. (2015). Ukiukaji wa kanuni za upole katika *Mhanga nafsi yangu*: Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Kothari, C. (2004). *Research methodology*. (2nd edition). New Age Technology Press.
- Lakoff, R. (1973). *Logic of politeness: Or minding your p's and q's*. Katika C. Corum, T. Ceric Smith- Stark, & A. Wisner (Eds.), papers from the 9th regional meeting of the Chicago

- Linguistic Society. *Chicago Linguistic Society*, 292-305. *Open Journal of Modern Linguistics*, vol No. 3, September 23, 2013.
- Leech, G. (1983). *Principles of pragmatics*. London and New York: Longman, 250. Harcourt Brace.
- LeVine, A. R. (1982). *Gusii Funerals: Meanings of life and death in an Africa community*. National Science Foundation, 26-60.
- LeVine, A.R., & LeVine, B.B. (1977). *Nyansongo: A Gusii community in Kenya*. Six cultures series. New York: John Willey & sons.
- Machira, S. (2015). Uchambuzi wa mikakati ya upole kama inavyotumiwa na wahusika wakuu katika Tamthilia ya Mbaya Wetu. Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Massamba, D.P. B. Kihore, Y. M. Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mathooko, P.M. (2007). *Isimu jamii: Misingi na nadharia*. Nairobi: Njigua Books.
- Mayer, P. (1949). *The lineage principle in Gusii society*. International African Institute Memorandum no. 24. London: Oxford University Press.
- Muge, T. (2018). Uchanganuzi wa upole katika mazungumzo ya vipindi vya Sobetab Kapchi katika Idhaa ya KASS FM. Tasnifu ya uzamifu chuo kikuu cha Moi. *The Africa Premier Research Publishing Hub*, 3(1)
- Mugenda, O. (2003). *Research methods: Quantitative and qualitative approaches*; Acts Press Nairobi.
- Muharrem, E. (1990). Katika: Hajar Shahhoseiny. Differences between language and linguistics in the ELT classroom. *Theory and Practice in Language Studies*, 3
- Mwari, R. (2014). Mikakati ya upole katika vipindi vya runinga: Mawaidha na Bi. Msafwari katika runinga ya Citizen. Tasnifu ya uzamilikatika Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Neimeyer, R. A., & Gillies, J. (2006). Loss, grief, and the search for significance: Toward a model of meaning reconstruction in bereavement. *Journal of Constructivist Psychology*, 19(1), 31-65.
- Nerlove, S. B. (1969). *Trait dispositions and situational determinants of behavior among Gusii children of South-Western Kenya*. University of Nairobi, Kenya.
- Nkwera, F. (1989). *Sarufi na fasihi ya sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Noduoushan, Salami M. S. (2013). The social semiotics of funerary rites in Iraq. *International Journal of Language Studies*, 7(1), 79-102.
- Ochieng, R.W. (1986). *Kenya's people: People of South-Western Highlands-Gusii*. Nairobi: Evans Brothers.
- Ochomba, N. (2015). The effectiveness of Egesa FM in the uptake of family planning by women in Kisii county. Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Omosa, F. (2015). Tasfida kama mkakati wa upole: Uwiano wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Owino, M. (2011). Uchanganuzi wa matini tuele ya nyimbo za Faustine Munish: Mtazamo wa nadharia ya upole. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

- Redmond, Mark V. (2015). Face and politeness theories. *English technical reports and white Papers*. 2. Retrieved from <http://lib.dr.iastate.edu/engl-reports/2>
- Sara Mills (2002). *Rethinking politeness, impoliteness and gender identity eds*. Litoselliti L and Sunderland J. Cambridge: Cambridge University Press.
- Sara Mills (2003). *Gender and politeness*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Scollon, R and Scollon, S. (1995). *Intercultural communication: A discourse approach*. Oxford: Ma: Blackwell publishing ltd.
- Searle, J. (1976). *Speech acts*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Spencer-Oatey, H. (2000). *Cultural speaking: Managing rapport through talk across cultures*. London: Continuum.
- Thomas, J (1995). *Meaning in interaction: An introduction to pragmatics*. New York: Longman Group Ltd.
- Troike, M. S. (2003). *The ethnography of communication: An introduction* (3rd edition). Blackwell publishing Ltd.
- TUKI (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. Dar es Slaam: TUKI.
- TUKI (2006). *English swahili dictionary* (3rd edition). Dar es Salaam: TUKI.
- Van Dijk, T. (2005). Multidisciplinary CDA. Katika Edds. Wodak, R. & Meyer, M. *Methods of critical discourse Analysis: Introducing qualitative methods*. London: Sage.
- Walibora, K. (2014). *Mbaya wetu*. Nairobi: Moran (E.A) Publishers Ltd.
- Walubengo, A. (2010). *Suala la upole katika jando ya jamii ya Wabukusu*. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya methali*. Nairobi: Focus Books.
- Wardhaugh, R. (2002). *Sociolinguistics: An introduction to language and society* (4th Edition). London: Blackwell Publishers.
- Watts, R. (2003). *Politeness*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Watts, R. et al. (2005). Politeness theory and relational work. *Journal of politeness Research, Language, Behaviour and Culture*, 1(1), 9-33.
- William M.K. (2005). Research methods knowledge base. Imetolewa kwa <https://libguides.usc.edu/writingguide>
- Williams, T. R. (2006). Linguistic politeness in expressing condolences: A case study. *RASK: International Journal of Languages and Linguistics*. Odense, Denmark: Odense University Press, 45-62.
- Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press.